# Utunzaji Bora wa Mbuzi wa Maziwa

---

SUA – EPINAV DAIRY GOAT PROJECT

2013

**Kitabu Hiki Kimetayarishwa na Washiriki wa Mradi wa Mbuzi wa Maziwa**
Prof. G. C. Kifaro
Prof. L. A. Mtenga
Prof. A. A. Kassuku
Prof. E. E. Ndemanisho
Prof. E. N. Kimbita
Dr. G. Msalya
Dr. D. E. Mushi
Dr. R. A. Max

**Kimehaririwa na:**
Prof. L. R Kurwijila
Prof. G. C. Kifaro
Dr. G. Msalya

**ISBN 978 - 9987 – 9673 – 4 – 6**

**Kimechapishwa na:**
Mradi wa Kukuza teknolojia za Mbuzi wa Maziwa
(Dairy Goats technologies),
Programu ya Ubunifu na Uwezeshaji wa Matumizi ya Rasilimali za Kilimo na Mifugo (EPINAV Programme),
Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo (SUA),
S. L. P. 3004, SUA
Morogoro – Tanzania
**Simu**: 255 023 – 26030970 au 0713 343 077
**Nukushi**: 255 023 – 26009770
**Barua pepe**: dasp@suanet.ac.tz, epinav@suanet.ac.tz na drpgs@suanet.ac.tz

Toleo Namba: TS2 - 64
**© EPINAV – SUA Dairy Goat Project, 2013**

# UTANGULIZI

## Sehemu ya kwanza

Katika sehemu ambazo ni vigumu kufuga ngombe wa maziwa na kwa wakulima wenye upungufu wa rasilimali au nyenzo za kujiendeleza, mbuzi wa maziwa ni muhimu katika kujibu maswala ya lishe bora na kipato. Familia hupata maziwa hasa kama kuna watoto au wazee ambao kwao maziwa ni ya lazima, kipato cha familia huongezeka, pamoja na faida nyingine nyingi kama vile mbolea kwa ajili ya bustani, nyama na ngozi. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo mbuzi wa maziwa wanapata umaarufu kwa kasi kubwa. Hii ni kutokana na faida zilizotajwa hapo juu pamoja na urahisi uliopo katika kuwafuga wanyama hawa ikilinganishwa na ng'ombe.

Utaalamu na elimu juu ya utunzaji bora wa mbuzi hawa haujaenea kiasi cha kutosha katika taifa letu. Tangu mwaka 1994, Idara ya Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji (DASP) ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), imekuwa ikiandaa vijitabu mbalimbali juu ya utunzaji wa mbuzi wa maziwa hususani kuhusiana na ulishaji, afya, uzalishaji na utunzaji wa kumbukumbu. Vijitabu hivi vimekuwa vikiandaliwa kwa ajili ya wafugaji wa mbuzi wa maziwa katika miradi mbalimbali inayofadhiliwa na shirika la maendeleo ya kimataifa la Norway (NORAD). Kwa kutambua maendeleo yaliyopatikana kati ya wakati huo na sasa katika swala zima la mbuzi wa maziwa ikiwa ni pamoja na ongezeko la wafugaji nchini, idara imetayarisha kitabu hiki kikiwa ni boresho la machapisho ya awali.

Kitabu hiki kinatoa mwongozo wa ufugaji bora kwa wafugaji wote wa mbuzi wa maziwa nchini. Ni matarajio yetu kuwa, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayojihusisha na uendelezaji wa mbuzi wa maziwa, mabibi na mabwana shamba watakitumia

kitabu hiki kuwaelimisha wafugaji katika maeneo wanayotoa huduma ya ugani.

## Sehemu ya pili

Kitabu ni maboresho vitabu vya awali. Mabadiliko yamefanyika katika vielelezo na maelezo kuhusu uzalishaji, uwekaji kumbukumbu na afya ya mbuzi wa maziwa, kwa lengo la kuufanya ujumbe umfikie msomaji/mfugaji kwa urahisi zaidi. Toleo hili limefadhiliwa na programu ya Ubunifu na Uwezeshaji wa Matumizi Bora ya Rasilimali na Kuongeza Thamani ya Mazao ya maliasili na Kilimo (SUA – EPINAV Programme, 2011 – 2014).

**G. C. Kifaro (2013)**

# YALIYOMO


| SURA | UKURASA |
|---|---|
| Utangulizi | iii |
| **Sehemu ya kwanza: Mabanda, ulishaji na mambo mengine ya utunzaji bora** | **1** |
| Maana ya utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa | 2 |
| Mabanda ya mbuzi wa maziwa | 4 |
| Lishe na ulishaji bora wa mbuzi wa maziwa | 11 |
| Mambo muhimu katika utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa | 19 |
| **Sehemu ya pili: Uzalishaji na Uwekaji kumbukumbu** | **29** |
| Upandishaji wa mbuzi jike | 30 |
| Uzalishaji wa mbuzi wa maziwa | 34 |
| Matatizo ya kuzaliana kiukoo | 38 |
| Kuchagua mbuzi bora kundini | 41 |
| Uwekaji wa kumbukumbu | 43 |
| **Sehemu ya tatu: Afya ya mbuzi wa maziwa** | **49** |
| Dalili za mbuzi mgonjwa | 50 |
| Athari za minyoo, kupe na ndorobo | 53 |
| Magonjwa hatari yanayoambukiza | 58 |
| Magonjwa mengine | 63 |
| Jinsi ya kukabiliana na matatizo ya dharura | 68 |
| Magonjwa ya watoto wa mbuzi | 71 |
| Matumizi ya dawa | 73 |

# SEHEMU YA KWANZA

## MABANDA, ULISHAJI NA MAMBO MENGINE YA UTUNZAJI BORA WA MBUZI WA MAZIWA

## SURA YA KWANZA

# Maana ya utunzaji Bora wa Mbuzi wa Maziwa

Ni wazi kuwa kila mwenye mfugo au mifugo anao ujuzi fulani wa utunzaji wa mifugo yake. Anafahamu kuwa bila kuwalisha, kuwatibu wanapokumbwa na maradhi, kuwakinga na wanyama wakali na kadhalika hawezi kuendelea kuwa na mifugo hao, na hata akiwa nao, hawatakuwa katika hali ya kuridhisha. Kwa wenye mifugo, uzalishaji ni ile namna ya kutekeleza yote yahusuyo uhai wa mifugo hiyo na uzalishaji wake. Kuna wafugaji wanaothamini hali ya kuwa na idadi kubwa ya mifugo bila kujali shibe wala afya nzuri ya mifugo yao, matokeo yake huwa na mifugo iliyodhoofu, yenye ukuaji hafifu, isiyozalisha kiasi cha kutosha (mfano maziwa kidogo) na mara nyingi hupoteza mifugo kwa vifo. Kuna wafugaji wengine ambao ingawa wangependa kuwa na mifugo mizuri na yenye kutoa mazao mazuri, hujikuta wanashindwa kufikia malengo yao kutokana na kutofahamu mambo muhimu ya kufanya au hukosa namna ya kukabiliana na matatizo mbalimbali yaikumbayo mifugo yao. Mfugaji bora hupaswa kutambua namna bora ya kutunza mifugo yake na jinsi ya kuzuia na kukabiliana na matatizo yawezayo kuikumba mifugo yake.

"Utunzaji bora" humaanisha kuhakikisha kuwa mnyama anapata chakula cha kutosha na kilicho bora, anatunzwa kwenye mazingira safi na yenye usalama, anakingwa na maradhi na maadui wengine wa mwili kama vile kupe, viroboto, minyoo, na anapata huduma nyingine zote muhimu zikiwemo kupunguzwa kwato zilizozidi na kusafishwa au kuoshwa. Utunzaji bora pia unahusha shughuli nyingine zote anazoweza kufanya mfugaji katika kuongeza ufanisi

wa uzalishaji wa mifugo yake. Mifano ya shughuli hizi ni kama ifuatavyo:

- Kupangilia namna ya kuzaliana kwa mifugo ili kusitokee kuzaliana kiukoo, kusitokee uzalishaji hovyo kipindi chote cha mwaka na kutumia madume yaliyochaguliwa kuendeleza kizazi bora kulingana na malengo ya ufugaji.
- Kupangilia namna ya kuvitunza vitoto mpaka vinapoachishwa maziwa kulingana na lengo la ufugaji.
- Kuhasi madume yasiyochaguliwa kuendeleza kizazi bora.
- Kukata pembe ili kuzuia kuumizana kwa mifugo au kuwaumiza wanaoihudumia na kupunguza mahitaji ya nafasi hasa kwenye mabanda.
- Kupunguza idadi ya mifugo kulingana na uwezo wa kuwatunza, na mengineyo.

**Utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa ulioelezwa katika kitabu hiki utazingatia yafuatayo:**

- Mabanda bora ya mbuzi
- Lishe na ulishaji bora wa mbuzi wa maziwa
- Huduma za siku hadi siku katika utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa
- Uzalishaji wa mbuzi wa maziwa
- Uwekaji na utunzaji wa kumbukumbu za mbuzi wa maziwa na
- Afya bora ya mbuzi wa maziwa

# Mabanda ya Mbuzi wa Maziwa

## Utangulizi

Ingawa mbuzi wa maziwa anaweza kulishwa kwa kupelekwa mbali na nyumbani kwa mfugaji, huhitaji hifadhi wakati wa usiku au mapumziko wakati wa kungojea kukamuliwa, akiwa mgonjwa au akingojea kuzaa. Mara nyingi mbuzi wa maziwa hutunzwa na kulishwa nyumbani. Hivyo ni muhimu kuwa na banda au nyumba ambayo imejengwa kwa ubora unaokubalika.

## Zifuatazo ni sababu za mbuzi kujengewa banda au nyumba

Sababu hizi zinazingatia ufugaji wa ndani wakati wote yaani mbuzi kukatiwa malisho na kupewa maji nyumbani bila kulazimika kwenda machungani au kutumia muda mfupi sana machungani ambapo pia ni karibu sana na nyumbani.

a) Usalama wa mbuzi dhidi ya wezi na wanyama wakali kama mbwa mwitu, chui, fisi na simba.
b) Mbuzi wakifungiwa watakuwa na nafasi ndogo ya kuharibu mazingira hata kama wataachwa bila mchungaji.
c) Ni rahisi kuwatenga mbuzi katika makundi mbalimbali ya umri na jinsia na kuwapa huduma tofauti kulingana na mahitaji yao.
d) Ni rahisi kukusanya mbolea (kinyesi, mkojo na masalia ya nyasi na malisho).
e) Ni rahisi kuepukana na magonjwa yawezayo kuambukizwa toka kwenye makundi ya jirani, au kutokana na mabadiliko

ya hali ya hewa pamoja na mazingira kwa ujumla. Hii ni pamoja na kupunguza matatizo ya kupe na minyoo. Kwa ujumla, afya ya mbuzi huwa bora zaidi akifungiwa nyumbani ukilinganisha na anapopelekwa machungioni ili mradi banda liwe bora na linalofanyiwa usafi wa mara kwa mara.

Kwa kuzingatia mambo yaliyodokezwa hapo juu, banda la mbuzi wa maziwa ni lazima lijengwe kwa kuzingatia ubora.

## Sifa za banda la mbuzi wa maziwa ni kama ifuatavyo:

(a) Liingize mwanga wa kutosha
(b) Liingize hewa ya kutosha
(c) Lizuie upepo mkali au maji kuingia
(d) Liwe na sehemu tofauti kwa ajili ya majike, madume na watoto wa mbuzi
(e) Liwe na sakafu nzuri ili mbuzi wawe na mahali pazuri pa kulala
(f) Liwezeshe shughuli za usafi kufanyika kwa urahisi
(g) Lisiwe linakaribisha ukusanyaji wa vumbi, matope, kinyesi na mkojo ili kuzuia ueneaji wa magonjwa (Tazama Vielelezo Na. 1 na 2)
(h) Liwe na sehemu ya kukamulia
(i) Liwe na hori na mahali pa kuwekea maji (Tazama Kielelezo Na. 2).
(j) Lisipitishe baridi kali



**Kielelezo Na. 1. Banda baya**

Banda baya huruhusu chakula cha mbuzi kuchanganyika na kinyesi, mkojo na uchafu mwingi, huwa na matatizo ya wadudu na magonjwa huweza kumkumba mbuzi na kusababisha utoaji mdogo wa maziwa.



**Kielelezo Na. 2. Banda zuri**
Ni muhimu kwa ajili ya mbuzi wenye afya nzuri, maziwa mengi na ni rahisi kukusanya mbolea

## Mgawanyo wa banda la mbuzi

Kama mfugaji ana uwezo, banda liwe na sehemu zifuatazo:

(a) **Vyumba vya majike**: Banda liwe na sehemu ya kuweka majike. Kila chumba kiwe na majike 3 hadi 4. Kwa wastani, kila mbuzi mkubwa anahitaji eneo la mraba mita 1.3 kwa 1.0.

(b) **Vyumba vya watoto wa mbuzi**: Hii ni sehemu ya lazima ili watoto wasiwanyonye kiholela mama zao. Kwa wastani chumba cha eneo la mraba mita 3.0 kwa 2.0 kinatosha kwa watoto wa mbuzi 4 hadi 6. Kusiwe na mazingira ya unyevunyevu kwani vifo vingi vinaweza kutokea.

(c) **Chumba cha dume:** Kama mfugaji ni mtunzaji wa dume kwa niaba ya wenzake, basi lazima awe na chumba pekee cha dume. Ni vizuri zaidi kama dume angekuwa na banda lake mwenyewe mbali kidogo na banda la majike. Chumba hiki au banda liwe na nafasi kubwa inayotosha dume na majike 3 kwa wakati mmoja. Majike yataletwa kwenye chumba hiki wakati wa kupandisha.

(d) **Stoo:** Banda liwe na sehemu ya kuhifadhia majani na vyakula vya mifugo.

| |
|---|
| KUMBUKA: UKUBWA WA BANDA UTATEGEMEA UWEZO WA MFUGAJI, KIASI CHA MBUZI ALIONAO NA MIPANGO YAKE YA BAADAYE |

## Mahali pa kujenga banda la mbuzi

Zifuatazo ni sifa za sehemu inayofaa kujenga banda la mbuzi:

(a) Iwe mbali kidogo na nyumba za kuishi watu.

(b) Iwe imeinuka kidogo ili mtiririko wa maji ya mvua, kinyesi na mkojo uwe rahisi.

(c) Iwe sehemu ambayo harufu haiendi upande wa nyumba wanakoishi watu.

## Vifaa viwezavyo kutumika katika ujenzi wa banda la mbuzi

Aina ya vifaa vya kutumia kujengea banda la mbuzi vinategemea sana uwezo wa mfugaji. Mfugaji anaweza kutumia vifaa na vitu vinavyopatikana kwa urahisi kwenye eneo lake.

(a) **Sakafu:** Ziko aina nne za sakafu zinazoweza kutumika katika banda la mbuzi

(i) **Sakafu ya udongo**: Ndiyo yenye gharama ndogo kuliko zote. Lakini ni lazima kutandika nyasi mara kwa mara ili mbuzi wapumzike vizuri.

(ii) **Sakafu ya mawe na kokoto:** Aina hii ni nzuri kama mawe na kokoto vitapangwa vizuri ili mbuzi wasiumie kwato na wapate kulala vizuri.

(iii) **Sakafu ya sementi:** Hii ni sakafu nzuri. Iwe na mwinuko mdogo ili kuzuia maji na mkojo vizisituame. Majani yatandikwe mara kwa mara kupunguza baridi ya sakafu. Hata hivyo sakafu ya aina hii ni gharama kubwa.

(iv) **Sakafu ya chaga za mbao:** Mita 0.5 hadi 1.0 juu ya ardhi. Ndiyo sakafu nzuri na inayopendekezwa zaidi ya zote. Mbao zitenganishwe kidogo kuruhusu kinyesi na mkojo kudondoka chini lakini nafasi kati ya ubao na mwingine izingatie ukubwa na nyayo za mbuzi.

(b) **Kuta:** Ziwe imara na zenye madirisha ya kutosha. Zaweza kujengwa kwa mbao, nguzo na mbao au mabanzi au za matofali.

(c) **Paa:** Sifa kubwa ya paa ni uwezo wa kuzuia mvua na jua kali. Banda la mbuzi laweza kutengezwa kwa nyasi, makuti, majani ya migomba na hata mabati.

(d) **Hori la chakula na ndoo ya maji:**

- Hori lijengwe kwa kutumia mbao
- Liwe na sehemu tatu maalum kwa ajili ya kulishia majani, pumba na mchanganyiko wa madini
- Lakini pia, majani yanaweza kutundikwa kwa kamba ndani ya banda au kwenye chaga zilizojengwa rasmi kwa shughuli hiyo.
- Ndoo itundikwe karibu na hori na iwe na maji wakati wote.

## Utunzaji bora wa banda la mbuzi

Ili kudumisha ubora na usafi wa banda na kujali afya ya mbuzi wakati wote, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

a) Kufagia na usafi wa jumla wa banda mara kwa mara

b) Kupiga au kunyunyiza dawa ya kuua wadudu na viroboto mara kwa mara

c) Kulifanyia banda matengenezo kila inapohitajika na hasa kwenye paa

d) Mbolea iondolewe mara kwa mara na kuwekwa sehemu maalum ili kupunguza harufu mbaya katika banda.

SURA YA TATU

# Lishe na Ulishaji Bora wa Mbuzi wa Maziwa

## Maana ya lishe bora

Lishe bora ni kumpatia mbuzi chakula bora chenye viinilishe vyote muhimu. Kiasi cha kulisha hutegemea uzito wake, hali ya utoaji maziwa au hali ya kawaida ya mbuzi. Mbuzi watoto, wanaotoa maziwa kwa wingi na wale wenye mimba walishwe vizuri.

## Faida za lishe bora

Zipo faida nne muhimu za lishe bora:

(a) Mbuzi kukua kwa haraka
(b) Mbuzi hutoa maziwa mengi na yenye virutubisho vyote muhimu kwa lishe ya mtoto wake na wanadamu
(c) Mbuzi hupata kinga dhidi ya maradhi
(d) Mbuzi huchangamka na kujisikia mwenye furaha.

## Viiniilishe muhimu katika chakula cha mbuzi wa maziwa

Chakula bora cha mbuuzi kitakuwa na viinilishe muhimuni vitano:

(a) Nguvu
(b) Protini
(c) Madini
(d) Vitamini na
(e) Maji

Umuhimu wa viinilishe hivi kwa mbuzi wa maziwa ni kama ifuatavyo:

(a) Nguvu
  (i) Hutunza joto la mwili wa mbuzi
  (ii) Humwezesha mbuzi kutembea, kumpa nguvu ya kula chakula na huuwezesha mwili wa mbuzi kufanya kazi vizuri
  (iii) Kudumisha mwili (kuupa uhai)

(b) Protini
  (i) Hujenga mwili
  (ii) Husaidia katika utengenezaji maziwa
  (iii) Huongeza kinga ya mbuzi dhidi ya maradhi
  (iv) Husaidia katika uzazi na kudumisha mwili kwa ujumla
  (v) Hutumika kuukarabati mwili.

(c) Madini
Baadhi ya shughuli muhimu za madini mwilini ni kama zifuatazo:
  (i) Huhusika katika ujenzi wa mifupa na meno
  (ii) Huungana na madawa ya mwili yanayohusika na usagaji au uyeyushaji wa chakula.
  (iii) Hufanikisha kazi mbalimbali za mwili kama kukaza na kulegeza misuli
  (iv) Huyeyusha na kuandaa viinilishe vingine kwa ajili ya matumizi mwilini na
  (v) Huhusika katika utengenezaji wa maziwa.

(d) Vitamini
Vitamini humsaidia mnyama:
  (i) Kuona Vizuri
  (ii) Kuzaliana vizuri na
  (iii) Kujilinda na maradhi mbalimbali

(e) Maji

Kwa kawaida sehemu kubwa ya mwili wa mnyama ni maji. Hivyo mnyama huhitaji maji ya kutosha kila wakati. Kazi muhimu za maji ni tano:

(i) Kuhusika katika kuyeyusha chakula tumboni
(ii) Kuhusika katika kusafirisha viinilishe mwilini
(iii) Kuhusika kwenye utoaji wa mabaki na makapi ya chakula kilichotumika mwilini
(iv) Kuhusika katika kutunza joto la mwili na
(v) Kuhusika katika utengenezaji wa maziwa.

## Vyanzo vya viinilishe na vyakula vya mbuzi

Viinilishe hupatikana katika vyakula vya aina mbalimbali anavyokula mbuzi. Ifuatayo ni mifano ya vyakula vya mbuzi:

(i) Nyasi
(ii) Mikundekunde
(iii) Majani ya miti ya aina mbalimbali
(iv) Mabaki ya mimea baada ya kuvuna mazao
(v) Mashudu (pamba na alizeti)
(vi) Pumba za mahindi
(vii) Chumvi, chokaa na madini mchanganyiko.

Vyakula hivi hutofautiana katika ubora na utoaji wa viinilishe mbalimbali kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali 1. Aina za viinilishe katika vyakula mbalimbali vya mbuzi**

| Aina ya vyakula | Viinilishe vinavyopatikana kwa wingi |
|---|---|
| **Nyasi:**<br>Guatemala<br>Ngugu<br>Setaria na nyinginezo | Nguvu, madini na vitamini |
| **Mimea jamii ya kunde:**<br>Lukina<br>Sesbania<br>Fiwi na nyinginezo | Protini, nguvu na madini |
| **Nafaka:**<br>Mahindi<br>Mtama<br>Pumba na nyinginezo | Nguvu na madini |
| Chumvi, chokaa na madini mchanganyiko | Madini kama (Kalisiumu, Fosiforasi na mengineyo) |
| Dagaa na mabaki ya samaki | Protini na madini |

## Mahitaji ya chakula kwa siku na ulishaji

### *Uwezo wa mbuzi kula chakula*

Mbuzi ana uwezo wa kula chakula asilimia tatu hadi sita ya uzito wa mwili wake kila siku. Hata hivyo uwezo huu hutegemea na hali halisi ya mbuzi pamoja na hali ya uzalishaji wake.

## Namna ya ulishaji

(a) Safisha vyombo vya kulishia kila siku
(b) Lisha mbuzi malisho safi na makavu
(c) Lisha vyakula/aina zote za viinilishe kwa mfano: nyasi, mikundekunde, majani ya miti na mabaki ya jikoni

(d) Katakata majani kabla ya kuwalisha mbuzi ili kupunguza upotevu wa majani
(e) Walishe mbuzi angalau mara tatu kwa siku na kwa muda ule ule.

## Ulishaji wa mbuzi katika makundi mbalimbali

Mbuzi watengwe na kulishwa katika makundi matano kama ifuatavyo:

(a) Mbuzi wadogo wanaokua
(b) Mbuzi majike wenye mimba
(c) Mbuzi majike waliozaa na wanakamuliwa
(d) Mbuzi majike waliokaushwa, wasiokuwa na mimba
(e) Mbuzi madume wanaotumika kupandisha.

## Sababu za kuwatenga mbuzi wa maziwa kwenye makundi ya ulishaji

Mahitaji ya chakula kwa kundi moja ni tofauti na yale ya kundi jingine. Hivyo ni vema kupanga vizuri ulishaji bora wa kila kundi na kuzingatia utengaji huu muhimu.

## Namna ya kulisha makundi mbalimbali ya mbuzi wa maziwa

(a) **Watoto wa mbuzi:** Ni muhimu kwa watoto wa mbuzi kukaa na mama zao wiki ya kwanza baada ya kuzaliwa. Hii ni kwa sababu kuu mbili: Moja, ni lazima watoto wa mbuzi wapate maziwa ya mwanzo yaani dang'a au kolostram kwa ajili ya kinga dhidi ya magonjwa na pili ni kuwawezesha waweze kukua haraka na barabara kupitia maziwa ya kutosha siku za mwanzo za uhai wao.

Baada ya wiki ya kwanza, watoto wa mbuzi wanaweza kukuzwa wa njia mbili

(i) Kunyonya kwa muda kutoka kwa mama yao kila siku. Ziko namna tatu za kunyonyesha na mfugaji anashauriwa kuchugua mmojawapo kulingana na hali halisi ya wakati huo.

- Mtoto akae na mama yake usiku mpaka asubuhi. Asubuhi watenganishwe na mama akamuliwe jioni.
- Mtoto akae na mama yake mchana kutwa mpaka jioni. Watenganishwe jioni na mama akamuliwe asubuhi na au
- Mtoto anyonye asubuhi na jioni kila baada ya mama kukamuliwa na kuondoa maziwa machache.

| |
|---|
| **KAMA ZITAZINGATIWA, TARATIBU HIZI TATU NI NZURI SANA NA ZITAPUNGUZA VIFO VYA WATOTO WA MBUZI** |

**Kumbuka:** Watoto wa mbuzi wapewe majani, chakula cha mchanganyiko na maji wakati wote. Waachishe kunyonya wafikiapo uzito wa kilo **8** hadi **10**.

(ii) Kumtenga mtoto na mama yake na kumlisha maziwa kwa kutumia chupa au ndoo.

- Juma la pili baada ya kuzaliwa, mtoto apewe nusu lita ya maziwa mara mbili kwa siku (asubuhi na jioni).
- Maziwa yaongezwe pole pole hadi yafikie lita moja na nusu kwa siku mpaka wiki ya nane. Kwa kiasi chochote cha maziwa anachopewa kwa siku nusu iwe asubuhi na nusu nyingine jioni.
- Baada ya wiki nane hadi ifikapo wiki ya kumi na mbili au mtoto afikiapo uzito wa kilo 8 – 10, kiasi cha maziwa kwa siku kipunguzwe kidogo kidogo.
- Baada ya muda huo mtoto wa mbuzi anaweza kuachishwa kunyonya na inashauriwa kuanza kumpa

**Kumbuka:** Baada ya kuachishwa ziwa, watoto wapewe chakula chenye nguvu na protini nyingi kwa muda wa wiki mbili ili wasipungue uzito.

| |
|---|
| **NJIA HII NI NZURI TU KAMA CHUPA AU NDOO ZINAZOTUMIKA KULISHIA WATOTO ZITAWEKWA KATIKA HALI YA USAFI WAKATI WOTE** |

**(b) Mbuzi katika makundi mengine**

(i) Walishwe majani na nyasi za kutosha

(ii) Wapate majani ya mikundekunde au ya miti yenye protini nyingi

(iii) Wapewe pia chakula kiasi cha mchanganyiko

Kwenye Jedwali Na. 2., mfano wa kiasi cha chakula anachohitaji mbuzi kwa siku.

Jedwali 2. Mahitaji ya chakula cha mbuzi kwa siku

| Kundi la mbuzi | Uzito wa mbuzi (Kilo) | Kiasi cha chakula (Kilo) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nyasi na majani | Majani ya kabichi au koliflawa | Chakula mchanganyiko | Majani makavu |
| Mbuzi wenye mimba | 20 | 0.1 | 1.0 | 0.7 | 0.8 |
| Mbuzi waliozaa | 30 | 0.3 | 2.2 | 0.9 | 1.2 |
| Wanaotoa maziwa | 20 | 0.2 | 1.0 | 0.8 | 0.9 |
| Mbuzi waliokaushwa, | 30 | 0.4 | 2.8 | 1.0 | 1.4 |
| Wasiokuwa na mimba | 20 | 4.0 | - | - | 0.6 |
| | 30 | 5.0 | - | - | 1.0 |
| | 40 | 6.0 | - | - | 1.2 |

## Utengenezaji wa chakula cha mchanganyiko kwa ajili ya mbuzi wa maziwa

Chakula cha mchanganyiko huweza kutengenezwa kwa kuchanganya kilo 70 za pumba, kilo 29 za mashudu ya pamba au majani makavu ya miti yenye protini nyingi kama vile lukina na kilo moja ya chokaa au madini machanganyiko. Kulingana na hali halisi na mazingira, pumba peke yake itatosha kuwa chakula cha nyongeza kama itakuwa vigumu kupata mashudu. Na endapo kwa bahati mbaya pumba hazitapatikana kabisa na hivyo kukosa uwezekano wa chakula cha mchanganyiko, mfugaji anapaswa kuhakikisha kuwa mbuzi wake wanapata nyasi nzuri za kutosha, majani ya miti ya aina ya mikunde, chumvi na chokaa kidogo.

SURA YA NNE

# Mambo Muhimu Katika Utunzaji Bora wa Mbuzi wa Maziwa

## Mambo muhimu katika utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa siku hadi siku

Kuna mambo muhimu ya kuzingatia yafuatayo katika utunzaji bora wa mbuzi:

- Huduma zinazotakiwa wakati wa kuzaa
- Kuhasi madume
- Kukata kwato
- Kukata pembe
- Kukamua na matumizi ya maziwa

## Huduma zinazotakiwa wakati mbuzi akizaa

(a) **Kila mfugaji anapashwa kuzifahamu dalili za mbuzi anayekaribia kuzaa. Nazo ni kama zifuatazo:**

Wiki sita hadi moja kabla ya mbuzi kuzaa kiwele hupanuka na kujaa maziwa. Anapokaribia sana kuzaa dalili zifuatazo zitaonekana:

(i) Kiwele hudondosha maziwa
(ii) Mbuzi kutotulia na kuvutavuta majani yaliyotandikwa akitumia miguu yake ya mbele
(iii) Kama yuko kwenye kundi, anaweza kujitenga na wenzake
(iv) Mbuzi huonyesha upendo mkubwa kila akikaribiwa na mtu

(v) Mbuzi hutokwa na ute kwenye uke

(vi) Mwishowe ataonekana kukaa chini huku akigeukia nyuma na kutoa sauti mara kwa mara na baadae ataonyesha uchungu mkubwa na kuanza kuzaa. Chupa ya uzazi ikisha pasuka haitapita saa moja bila mbuzi kuzaa.

**(b) Baada ya dalili za mwanzo kuonekana vitu vifuatavyo vitayarishwe:**

(i) Dawa ya joto (Iodine) na dawa kusafishia vidonda.

(ii) Maji safi ya uvuguvugu

(iii) Majani makavu.

**(c) Maandalizi mengine kwa ajili ya mbuzi anayezaa**

(i) Mwandandalie mbuzi anayezaa mahali pasipo na upepo wala jua kali kwa ajili ya kuzaa na kupumzika

(ii) Pawe mahali safi na patulivu

(iii) Mara baada ya mbuzi kuzaa, apewe maji mengi kwa vile atakuwa amepoteza maji mengi wakati wa uzazi. Hii itamsaidia kuwa na maziwa mengi kwa ajili ya mtoto.

**(d) Mtoto wa mbuzi anapozaliwa**

(i) Kwa kawaida mbuzi hawana matatizo wakati wa uzazi, lakini wakati mwingine mtoto/watoto wanaweza kukwama.

(ii) Endapo mbuzi atashindwa kuzaa asaidiwe, lakini kabla ya kufanya hivyo, osha mkono kwa dettol au sabuni, hakikisha kucha zako zimekatwa na usiwe na vitu kama vile pete kwa kuwa vinaweza kumuumiza mbuzi.

(iii) Pata mipira ya kuvaa mikononi (glovu). Hizi zitakufanya kutomuumiza mbuzi na pia husaidia kujikinga na maambukizi ya magonjwa na hata kumkinga mbuzi.

(iv) Tambua sehemu za mtoto zinazojitokeza kwenye sehemu ya nje ya uzazi.

(v) Kama una wasiwasi kuwa kuna watoto zaidi ya mmoja, kuwa mwangalifu, hakikisha kuwa unatambua miguu ya mtoto utakayemsaidia kutoka kwanza.

(vi) Unapomsaidia mtoto anayezaliwa, fanya polepole na hakikisha unafahamu tatizo kabla ya kutumia nguvu zozote.

(vii) Anza kuvuta miguu ya mtoto wa mbuzi kwa uangalifu kichwa kikiwa mbele.

(viii) Unapomvuta mtoto, vuta wakati mbuzi anaposukuma mtoto na si vinginevyo.

**(e) Mtoto wa mbuzi akishazaliwa**

Mara nyingi baada ya kuzaliwa, mtoto hulambwa na mama yake ili kuukausha mwili wa mtoto wake. Hata hivyo, huduma zifuatazo ni muhimu kama mtoto wa mbuzi ataonekana kuhitaji msaada kwa namna iwayo yote:

(i) Kama mtoto ataonyesha dalili za kutokupumua sawasawa, ainuliwe juu kwa miguu ya nyuma na kutikiswa kidogo ili ashtuke na ataanza kupumua.

(ii) Watoto dhaifu wasaidiwe.

(iii) Mtoto akaushwe kwa kutumia majani makavu.

(iv) Weka iodine kwenye kikombe au chupa na tumbukiza kitovu cha mtoto.

(v) Mtoto apimwe uzito.

(vi) Mtoto awekwe sehemu yenye kivuli na kavu, pasiwe na joto au upepo mkali

(vii) Watoto wenye afya watasimama kati ya dakika 10 na 15 baada ya kuzaliwa na wataanza kutafuta chuchu.

(viii) Mtoto asaidiwe kunyonya kwa mama yake kama atashindwa kugundua mwenyewe.

(ix) Hakikisha mtoto ananyonya maziwa ya awali kati ya dakika 20 – 30 tangu alipozaliwa.

**Kuhusu kuhasi madume**

(a) Madume yote ambayo hayahitajiki kwa mbegu au upandishaji yahasiwe.
(b) Njia rahisi ya kuhasi madume itumike. Chombo maalumu cha kuhasia (burdizzo) ni rahisi kutumika.
(c) Madume yahasiwe kabla hayajafikia umri wa miezi mitatu.


## Umuhimu wa kukata kwato

(a) Kwato zikirefuka sana zina madhara yafuatayo:
  (i) Mbuzi hutembea kwa shida
  (ii) Kwato huoza kutokana na vijidudu vya maradhi ambavyo huweza kukaa kwenye sehemu za kwato zilizokunjamana na hivyo kuwa na unyevunyevu.
  (iii) Kwa ujumla humfanya mbuzi kuonekana vibaya.

(b) Mbuzi akipunguzwa kwato husimama vizuri, hutembea sawa sawa, kwato zake hubakia kavu daima na magonjwa ya kwato hupungua.
(c) Kufuatana na mahali anapotembea mbuzi (sakafuni, udongoni au kwenye nyasi) kwato huweza kukua haraka au pole pole. Mbuzi wakatwe kwato mara ziwapo ndefu (Tazama Vielelezo Na. 3 na 4).



**Kielelezo Na. 3.**
**Kwato zilizozidi**



**Kielelezo Na. 4.**
**Kwato zilizokatwa**

(d) Kisu kikali au mkasi vinaweza kutumika kukata kwato kwa kumshika mbuzi kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 5.



**Kielelezo Na. 5. Mbuzi akikatwa kwato mguu wa nyuma**

## Umuhimu wa kukata pembe

Wakati mwingine ni vizuri kukata pembe za mbuzi,

(a) Pembe za mbuzi zikiwa kubwa huweza kuleta matatizo yafuatayo:
   (i) Kuumizana kwa mbuzi
   (ii) Mbuzi huhitaji nafasi kubwa kwenye banda, katika sehemu ya chakula au ya kunywea maji.
   (iii) Pembe kubwa au ndefu sana ni mzigo kwa mbuzi.
   (iv) Sehemu ya chakula mwilini hutumika kukuza na kuzitunza pembe badala ya kutumika katika kazi nyingine za mwili.
   (v) Pembe ndefu zaweza kusababisha mbuzi aliyefungiwa malishoni kunasa na kukwama kwenye vichaka.

(b) Kwa mbuzi wadogo (umri wa siku tatu hadi wiki mbili) vianzio vya pembe vinaweza kuondolewa ili pembe zisikue. Vianzio hivyo vya pembe huweza kuondolewa kwa kuchoma sehemu za maoteo ya pembe kwa kutumia chuma cha moto.

(c) Kwa mbuzi wakubwa pembe huweza kuondolewa kwa kutumia msumeno, waya wenye makali au dawa maalumu (kemikali) kwa ajili ya kazi hiyo.

(d) Lakini ni vema mfugaji kupata ushauri kutoka kwa daktari wa mifugo kabla ya kufanya shughuli hizi.

## Ukamuaji na matumizi ya maziwa ya mbuzi

### Kanuni za kufuata katika ukamuaji bora wa mbuzi

**Zipo kanuni kuu tano kama ifuatvyo:**

(a) Mbuzi wawe katika hali ya usafi wa mwili kama ifuatayo:
   (i) Manyoya yaliyozidi urefu katika eneo la kiwele yapunguzwe mara kwa mara.
   (ii) Mbuzi apanguswe vizuri sehemu za kiwele kwa kutumia brashi laini ili kuondoa matope na vumbi.

(b) Patengwe mahali salama na safi mbali na sehemu ya kulala mbuzi wengine ili patumike kwa shughuli za kukamua tu.

(c) Mbuzi dume asiruhusiwe kujisogeza sehemu za kukamulia wakati wa ukamuaji kwa sababu mbili:
   (i) Huweza kumsumbua mbuzi jike
   (ii) Harufu ya mbuzi dume inaweza kuingia kwenye maziwa kwa urahisi

(d) Kabla ya kukamua kanuni tatu za usafi zifuatazo zizingatiwe:
   (i) Mkamuaji asafishe mikono yake kwa maji safi na sabuni.
   (ii) Kiwele kisafishwe kwa maji ya uvuguvugu (Kielelezo Na. 6).
   (iii) Chuchu zikaushwe kwa kitambaa safi.

(e) Maziwa yakamuliwe kwa ustadi pasipo kuvuta chuchu. Inawezekana kumkamua mbuzi kwa kugandamiza kidole cha kwanza dhidi ya dole gumba kama inavyooneshwa kwenye Vielelezo Na. 7 na 8.



Kielelezo Na. 6. Kusafisha kiwele



Kielelezo Na. 7. Kukamua kwa kugandamiza vidole na kutumia mikono yote

Hii ndiyo aina nzuri ya ukamuaji. Chuchu nene zinafaa zaidi kwa ukamuaji huu. Kwa vile chuchu za mbuzi ni ndogo, wakati mwingine itakuwa vigumu kutumia njia hii. Njia hii hutumika pia kwa ng'ombe.



**Kielelezo Na. 8. Kukamua kwa kuvuta chuchu**
Huu ni ukamuaji mbaya na huumiza chuchu.

## Vitendo baada ya kukamua maziwa

Baada ya kukamua maziwa, mambo yafuatayo yafanyike:

(a) Maziwa yachemshwe huku yakikorogwa kwa kijiko hadi yatokote kwa muda usiozidi dakika tano. Epuka kuunguza maziwa, huharibu viini lishe.

(b) Maziwa yapoozwe haraka katika chombo chenye maji baridi huku yakiwa yanakorogwa.

## Matumizi ya maziwa ya mbuzi

(a) Maziwa ya mbuzi yana matumizi sawa na maziwa ya ng'ombe. Yanaweza kutumika kwa ajili ya kunywa au kupikia chai au kahawa.
(b) Maziwa yauzwe kwa familia za jirani baada tu ya kutosheleza mahitaji ya familia ya mfugaji. Maziwa ya kuuza yawekwe kenye chupa au chombo kilicho safi.

Yapo matumizi mengine kadhaa mbali na yaliyotajwa hapo juu:
(a) Maziwa yakiachwa katika hali ya joto, huganda katika muda wa masaa 10 – 12. Njia hii ya kugandisha hutumika sana katika makabila mengi ya wafugaji wa Tanzania. Maziwa yaliyogandishwa yanaitwa MTINDI.
(b) Vilevile samli, jibini na siagi vinaweza kutengenezwa kutokana na maziwa ya mbuzi.

### Njia bora za kutengeneza mtindi

(a) Kuchemsha maziwa huku yakikorogwa kwa muda wa dakika tano.
(b) Kupooza maziwa katika sufuria lenye maji baridi.
(c) Kuweka kimea cha maziwa mgando kiasi cha kijiko kimoja cha chakula kwa kila lita moja ya maziwa.
(d) Kuhifadhi maziwa yaliyofunikwa sehemu yenye joto kidogo, mfano kwenye kabati usiku mzima.

**MTINDI UTAKUWA TAYARI KWA KUNYWEWA SIKU INAYOFUATA**

# SEHEMU YA PILI

## UZALISHAJI NA UWEKAJI KUMBUKUMBU

SURA YA TANO

# Upandishaji wa Mbuzi Jike

## Kumpandisha mbuzi jike kwa mara ya kwanza

Mifuko ya mayai huweza kuanza kutoa yai mbuzi jike akiwa na umri wa miezi 5 hadi 8. Lakini katika umri huo mbuzi haruhusiwi kupelekwa kwa dume kwa sababu ni mdogo sana na bado anahitaji kukua. Ni vigumu mbuzi wa aina hii kuweza kumlisha mbuzi mwingine tumboni. Matokeo ya kumpandisha mbuzi katika umri huo mdogo ni kutupa mimba, kushindwa kuzaa na/au kutoa maziwa kidogo mara baada ya kuzaa. Inasisitizwa mbuzi apandishwe akifika umri wa miezi 8 hadi 12 au baada ya kupata uzito unaoridhisha, yaani asilimia 50 – 60 ya uzito wa mbuzi mkubwa wa aina yake. Kwa chotara wa Kinorway tunashauri isiwe chini ya kilo 18. Ili uweze kufahamu uzito na/au umri wa mbuzi kuanza kuzalisha, ni muhimu kuweka kumbukumbu nzuri za upimaji uzito na tarehe za kuzaliwa. Mbuzi wanaokua kwa *matatizo kama vile kuugua mara kwa mara inashauriwa* wacheleweshwe kupandishwa.

## Upandishaji wa mbuzi jike baada ya kuzaa

Ni muhimu kufahamu kuwa mimba ya mbuzi huchukua siku 145 hadi 150 yaani miezi 5. Uamuzi juu ya lini kumpandisha utategemea unapendelea nini. Lengo la kufuga mbuzi wa maziwa linaweza kuwa:

- Kuzalisha maziwa mengi ya kutumia nyumbani na ziada kuuza.
- Kuzalisha watoto wa mbuzi ili wakuapo waweze kuuzwa na huku mbuzi wakitoa maziwa machache.

Aidha unaweza kuwa na lengo la kumfanya mbuzi azae mara moja kwa mwaka au mara tatu katika miaka miwili.

## Ili kufanikisha malengo hayo inabidi

(a) Kumpandisha mbuzi miezi 4 – 6 baada ya kuzaa ili aweze kuzaa mara moja kwa mwaka.

(b) Kumpandisha mbuzi miezi 2 – 3 baada ya kuzaa ili aweze kuzaa mara tatu katika miaka miwili.

## Dalili za mbuzi jike kuhitaji dume (kuwa kwenye joto)

Dalili za mbuzi jike mwenye joto ni kama zifuatazo:

- Sehemu ya nje ya uzazi (uke) huvimba kidogo na huwa nyekundu kuliko kawaida.
- Ulaji chakula na utoaji maziwa hupungua kidogo.
- Huwa na wasiwasi, hutikisatikisa mkia (hasa akimwona dume) na kupiga kelele.
- Hutokwa na ute sehemu za uke ambao huweza kudondokea hata miguu ya nyuma
- Hupenda kuwapanda mbuzi wengine au yeye kukubali kupandwa.

Joto la mbuzi huendelea kwa wastani wa siku mbili (masaa 48). Yai katika tumbo la uzazi la mbuzi hutoka saa 24 – 36 tangu joto linapoanza. Mbuzi apelekwe kwa dume mara dalili za joto zinapoonekana. Chunguza tena dalili za joto baada ya siku 19 – 21 kwa sababu si lazima mbuzi apate mimba anapopandwa mara ya kwanza. Asiporudia joto kuna uwezekano mkubwa kuwa amekwisha pata mimba. Ukiweka kumbukumbu za upandishaji utaweza kukadiria lini atarudia joto, na kama hakurudia basi unaweza kutabiri lini atazaa.

## Unaweza kupanga mbuzi wako azae lini

Ni vema kupanga muda mzuri wa kupandisha ili mbuzi wasizae wakati wa mvua nyingi na/au baridi kali sana. Ni rahisi kwa mbuzi wachanga kupata vichomi (nimonia) na kufa. Jedwali namba tatu linaelekeza namna ya kufuatilia mbuzi mpaka wakati wa kuzaa tangu tarehe ya kupandishwa.

**Jedwali 3. Tarehe ya kupandisha mbuzi wa maziwa na ya kutegemewa kuzaa**

| Kupandisha | Kuzaa | Kupandisha | Kuzaa |
|---|---|---|---|
| **Januari** 1 | **Mei** 30 | **Julai** 5 | **Desemba** 1 |
| • 6 | **Juni** 4 | 10 | 6 |
| • 11 | 9 | 15 | 11 |
| • 16 | 14 | 20 | 16 |
| • 21 | 19 | 25 | 21 |
| • 26 | 24 | 30 | 26 |
| • 31 | 29 | **Agosti** 4 | 31 |
| **Februari** 5 | **Julai** 4 | 9 | **Januari** 5 |
| 10 | 9 | 14 | 10 |
| 15 | 14 | 19 | 15 |
| 20 | 19 | 24 | 20 |
| 25 | 24 | 29 | 25 |
| **Machi** 2 | 29 | **Septemba** 3 | 30 |
| 7 | **Agosti** 3 | 8 | **Februari** 4 |
| 12 | 8 | 13 | 9 |
| 17 | 13 | 18 | 14 |
| 22 | 18 | 23 | 19 |
| 27 | 23 | 28 | 24 |
| **Aprili** 1 | 28 | **Octoba** 3 | **Machi** 1 |
| 6 | **Septemba** 2 | 8 | 6 |
| 11 | 7 | 13 | 11 |
| 16 | 12 | 18 | 16 |
| 21 | 17 | 23 | 21 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 26 | 22 | 28 | 26 |
| **Mei** 1 | 27 | **Novemba** 2 | 31 |
| 6 | **Octoba** 2 | 7 | **April** 5 |
| 11 | 7 | 12 | 10 |
| 16 | 12 | 17 | 15 |
| 21 | 17 | 22 | 20 |
| 26 | 22 | 27 | 25 |
| 31 | 27 | **Desemba** 2 | 30 |
| **June** 5 | **Novemba** 1 | 7 | **Mei** 5 |
| 10 | 6 | 12 | 10 |
| 15 | 11 | 17 | 15 |
| 20 | 16 | 22 | 20 |
| 25 | 21 | 27 | 25 |
| 30 | 26 | 31 | 29 |

SURA YA SITA

# Uzalishaji wa Mbuzi wa Maziwa

## Umuhimu wa uzalishaji katika mbuzi wa maziwa

Ni vizuri kufahamu kuwa:

- Kuna aina nyingi za mbuzi.
- Kila aina ya mbuzi ina uwezo tofauti wa kutoa maziwa, na
- Hata katika aina moja ya mbuzi kuna tofauti nyingi.

Hivyo, kufanya uchaguzi wa mbuzi bora ni jambo la lazima.

## Tofauti kati ya mbuzi wa kienyeji na mbuzi wa kigeni (mbuzi wa maziwa)


Tofauti hizo zimeainishwa katika Jedwali Na. 4

**Jedwali 4. Tofauti kati ya mbuzi wa kienyeji na mbuzi wa maziwa**

| Na. | Sifa | Mbuzi wa kienyeji | Mbuzi wa kigeni wa maziwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukuaji | Polepole | Haraka |
| 2 | Utoaji maziwa | Kidogo | Mengi |
| 3 | Uwezo wa kustahimili | Mkubwa | Mdogo |
| | • Joto | Mkubwa | Mdogo sana |
| | • Magonjwa na vimelea | Mkubwa | Mdogo sana |
| | • Lishe hafifu | | |
| 4 | Umbile | Dogo | Hutofautiana lakini wengi ni wakubwa |
| 5 | Rangi katika aina (breed) moja | Zinatofautiana sana | Wanafanana |

## Mbuzi wa maziwa wa kisasa na jinsi ya kuongeza damu yao katika mbuzi wa kienyeji

Mradi wa Mgeta umefadhiliwa na Shirika la Ushirikiano na Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa la Norway yaani NORAD. Mbuzi wanaofugwa Mgeta kwa mara ya kwanza waliletwa nchini mwaka 1983 na kutathminiwa kwa miaka 5 chuoni SUA. Baadaye walipelekwa Mgeta mwaka 1988. Tangu wakati huo, mbuzi hawa wamekuwa wakichanganywa na damu ya mbuzi wa kienyeji ili kuongeza uzalishaji wa maziwa wa mbuzi wa kienyeji. Mbuzi wa kienyeji hawawezi kutoa maziwa ya ziada zaidi ya yale yanayohitajika kumlisha mtoto wake. Lakini mbuzi wa kienyeji anaweza kuwa chanzo kizuri cha kuzalisha mbuzi wa maziwa. Wafugaji wachache wana uwezo wa kununua mbuzi chotara au asilimia kubwa kwa ajili ya maziwa. Namna ya kupandisha mbuzi wa kienyeji kwa kutumia madume ya kisasa (madume ya Norway) yaliyopo vijijini imeoneshwa katika Kielelezo Na. 9. Hivyo, unaweza kuongeza damu ya mbuzi wa kisasa kwa mbuzi wako. Kwa sasa wafugaji wachache wana uwezo wa kununua mbuzi chotara au wa kisasa kwa ajili ya maziwa.




**Kielelezo Na. 9. Namna ya kuchanganya damu kati ya mbuzi jike wa kienyeji na dume wa kisasa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa**

Maelezo: X = Kupandisha

Kadri utakavyoendelea kupandisha watoto kwa dume la kisasa ndivyo utakavyoongeza ubora wa mbuzi wako. Kama utakavyoona hapo baadae (Sura ya Saba), yakupasa kukumbuka kuwa kila mara jike chotara anapopandishwa litumike dume la kisasa tofauti na lile ambalo ni baba yake. Mbuzi wa asilimia 75 na kuendelea ni mbuzi wazuri kwa utoaji wa maziwa na wanaweza kupatikana katika ndani ya miezi 28 (miaka 2 na miezi 4) toka unapoanza kumpandisha mbuzi jike wa kienyeji.

Kuna aina nyingine za mbuzi wa maziwa kama vile Saanen na Toggenburg (kutoka Uswisi), Alpine (kutoka Uswisi na Ufarasa) na Anglo–Nubian (Chotara wa maziwa kwa damu za mbuzi wa Sudani, India, Uswisi na Misri). Mbuzi hawa wengi ni machotara na wanapatikana sehemu mbalimbali nyingine za nchi yetu ya Tanzania.

## Kanuni zinazofaa katika upandishaji

i. Kuendelea kutumia madume bora ya mbuzi wa kigeni au wa kisasa kwa majike yote yenye asilimia 100 damu ya kigeni ili kupata madume ya mbegu yanakayotumika kupandisha sehemu nyingine.

ii. Kutumia madume bora kwenye mbuzi wa kienyeji ili watoto wao (machotara) waweze kuwa mbuzi wa maziwa.

iii. Madume yote yenye damu ya kigeni chini ya asilimia 75 hayafai kwa kupandisha sababu wataleta ongezeko hafifu la damu ya kigeni katika watoto watakozaliwa. Hivyo wahasiwe na hatimaye kuchinjwa kwa ajili ya nyama.

iv. Madume yenye asilimia 75 hadi 94 yanaweza kuuzwa kwa watu ambao hawawezi kupata madume bora ya kigeni. Hao watawasaidia kuongeza damu ya kigeni katika makundi yao.

# Matatizo ya Kuzaliana Kiukoo

## Maana ya kuzaliana kiukoo

Katika jamii zote za wanyama kuzaliana kiukoo kwa uhusiano wa karibu hakuruhusiwi. Kwa mfano hairuhusiwi mbuzi jike kupandishwa kwa dume ambaye ni mtoto wake. (mama kwa mtoto) au dume kwa mbuzi jike ambaye ni mtoto wake (baba kwa mtoto) au hata watoto jike na dume waliozaliwa na wazazi hao hao.

## Madhara ya kuzaliana kiokoo

- Kwanza watoto wanaozaliwa wanaweza kuwa vilema au kufa wakiwa wachanga.
- Pili, watoto hao huzaliwa wakiwa dhaifu na hukua kwa matatizo sana.

## Jinsi ya kuliepuka tatizo la kuzaliana kiukoo

Mbuzi jike huwa tayari kupandishwa akiwa na umri wa miezi 8 – 12. Ina maana dume akikaa katika shamba au kijiji kwa zaidi ya mwaka mmoja uwezekano wa kuzaliana kiukoo ni mkubwa sana. Inashauriwa:


(a) Kubadili madume kila mwaka au

(b) Kuwa mwangalifu sana katika kutunza kumbukumbu za upandishaji kila mwaka na kuhakikisha kwamba mbuzi jike anapandishwa kwa dume asiyehusiana naye kiukoo. Kwa hali ya kawaida, si rahisi kufuata mpango huu. Hivyo,

(c) Madume wanaozaliwa shambani (Kijijini) waondolewe mara baada ya kuachishwa kunyonya.

## Mzunguko wa madume

Tumeona kuwa dume hawezi kutunzwa katika kundi moja kwa zaidi ya mwaka mmoja. Na kwamba, ni gharama kubwa sana kwa mfugaji kununua dume jipya kila mwaka. Ni dhahiri, kuna ulazima mkubwa wa kubadilishwa kwa madume. Uzoefu wa Mgeta na sehemu nyingine duniani umeonyesha kuwa mzunguko wa madume kila mwaka (au kila baada ya miezi 6) unaweza kutatua tatizo la kuzaliana kiukoo. Angalia Kielelezo Na. 10.




**Kielelezo Na. 10. Namna ya kuzungusha madume kuzuia kuzaliana kiukoo**

Mzunguko huu unawezesha madume kuwa na watoto katika vijiji vingi. Watoto bora wa madume hawa katika vijiji wachaguliwe kwa ajili ya upandishaji.

Hata hivyo kuna mambo ya muhimu ya kuzingatia katika kuhakikisha ufanisi wa mzunguko huu kama ifuatavyo:

(i) Ili dume aweze kutunzwa na kustawi ni vizuri na mfugaji aliyebeba dhamana ya kumtunza mmoja asaidiwe. Hivyo upandishaji ulipiwe kwa kiasi kitakachoamuliwa na wafugaji wenyewe kwa kuangalia mahitaji halisi ya wakati huo. Malipo hayo yatasaidia kununua chakula cha ziada kama pumba, madini na mengineyo na hata manunuzi ya dawa endapo dume ataugua.

(ii) Kila dume awe na kitabu au kadi kwa ajili ya kumbukumbu za dume mwenyewe (Kama vile namba yake, tarehe ya kuzaliwa, wazazi wake, chanjo na matibabu) na kuweka kumbukumbu za majike wote wanaopandishwa kwake.

(iii) Vijiji vitatu hadi sita vinaweza kushirikiana kutengeneza mzunguko wa madume. Muda wa dume kukaa katika kijiji kimoja unaweza kufupishwa mpaka miezi sita.

(iv) Chanzo cha madume ya kupandishwa kinaweza kuwa taasisi yoyote na/au kuchaguliwa kutokana na mbuzi bora wa wafugaji wenyewe.

(v) Baada ya dume kumaliza mzunguko wa vijiji bila matatizo, anaweza kuuzwa au kupelekwa kwenye mzunguko mwingine mbali na vijiji husika.

SURA YA NANE

# Kuchagua Mbuzi Bora Kundini

## Sifa za kundi bora

Kundi la mbuzi linalofugwa vizuri lina sifa zifuatazo:

- Vifo vya mbuzi ni vichache sana na hawaugui mara kwa mara
- Mbuzi wanakua na kuongezeka kwa haraka
- Mbuzi huanza kuzaa mapema na baadaye huzaa mara kwa mara na
- Mbuzi hutoa maziwa mengi.

## Ulazima wa kufanya uchaguzi wa mbuzi bora kundini

Ni muhimu mbuzi wote ambao hawakui na kuzaa upesi, wanaougua mara kwa mara na wanaotoa maziwa kidogo waondolewe katika kundi. Licha ya kukuletea hasara katika ufugaji, mbuzi hao wataendeleza kizazi kibaya katika kundi.

- Dume lazima achaguliwe kwa makini sana sababu "dume ni nusu ya kundi". Hii ina maana kuwa dume mmoja anatumika kwa majike yote uliyo nayo. Uchaguzi mbaya wa dume utaendeleza kizazi cha ovyo.
- Jike huzaa na kutoa maziwa. Jike asiyezaa mara kwa mara au asiyetoa maziwa ya kutosha huleta hasara.

## Sifa za mbuzi wazuri

### Sifa za dume bora

(a) Mwenye asilimia zaidi ya 90 ya damu ya kigeni (mbuzi wa Maziwa).

(b) Anayekua upesi, umbile kubwa (mgongo mpana na kiuno kikubwa). Aidha baba yake pia awe na mwili mkubwa.

(c) Mama yake (au dada zake) wawe watoaji wazuri wa maziwa.

(d) Sehemu zake za kiume ziwe kamilifu (zisizo na dosari) na awe na uwezo wa kupanda.

(e) Kwa ujumla awe mwenye afya bora.

## Sifa za jike Bora

(a) Anayekua upesi, ana kiuno kikubwa na tumbo kubwa la kumwezesha kula majani mengi.

(b) Awe anazaa mara kwa mara.

(c) Miguu yake ya nyuma iwe na nguvu, imenyooka na haijakaribiana ili kukipa kiwele nafasi.

(d) Awe na kiwele kikubwa na anayetoa maziwa mengi. Kiwele cha kulia na kushoto vifanane na asiwe na chuchu ndogo sana.

(e) Mwenye afya bora

SURA YA TISA

# Uwekaji wa Kumbukumbu za Mbuzi

## Faida za kuweka Kumbukumbu

- Kumbukumbu zinasaidia kuelewa nini la kufanya na lini. Kwa mfano:
  - Lini unategemea mbuzi apate joto ili apandishwe.
  - Lini mbuzi atazaa kama tarehe ya kupandishwa iliandikwa.
  - Lini kuwapa mbuzi dawa ya minyoo.

- Kumbukumbu za muda mrefu hutuonyesha mambo gani yanaleta faida au hasara na nini kifanywe kurekebisha au kuongeza ufanisi. Ina maana kuwa kumbukumbu ni njia mojawapo ya kuongeza ujuzi wa ufugaji.

- Kumbukumbu hutumika kufanya uchaguzi wa mbuzi mzuri (anayezaa sana, anayetoa maziwa mengi, anayekuwa upesi) na kufanya maamuzi mengine katika ufugaji.

- Ufugaji ni mradi sawa na mradi mwingine wowote. Inatubidi tufahamu matumizi ya fedha na mapato ili tuweze kukokotoa faida na hasara za utunzaji wa mbuzi.

- Wataalam watatumia kumbukumbu ili kutambua matatizo yaliyopo na hatimaye kuyatafutia ufumbuzi na ushauri.

## Jinsi ya kutofautisha mbuzi

Kabla ya kuanza kutunza kumbukumbu ni lazima uweze kuwatofautisha mbuzi kwa kuwapa vitambulisho. Unaweza kuwatofautisha mbuzi wako kwa njia zifuatazo:

- Kutumia majina. Mfano unaweza kuwaita mbuzi wako kwa majina ya Pili au Mtumba.
- Kwa kuwavalisha mbuzi kamba zenye namba shingoni.
- Kwa kuwawekea heleni zenye namba masikioni (Ear tags). Zipo heleni za plastiki na za chuma.
- Kwa kuwachanja namba upande wa ndani wa masikio kwa kutumia mashine maalum iitwayo tattoo na kupaka wino maalum kwa kazi hiyo.

## Aina ya kumbukumbu za kutunza

Kila mbuzi akiwa na kitambulisho unaweza kutunza kumbukumbu zake. Kuna kumbukumbu za aina nyingi lakini zifuatazo ni zile za muhimu na inafaa zitunzwe kwa uangalifu sana.

### 1. Kumbukumbu (rejista) ya uzazi

Kila mbuzi anayezaliwa inafaa aandikwe kwenye rejista kama inavyoonyesha kwenye mfano ufuatao.

| Tarehe ya kuzaliwa | Namba ya mbuzi | Jinsi (Me/Ke) | Aina (Breed) | Watoto kwa mzao | Baba | | Mama | | Uzito wa kuzaliwa | Menginey |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Namba | Aina | Namba | Aina | | |
| | | | | | | | | | | |

Me: Dume, Ke: Jike; Breed: Wa Kienyeji au Asilimia kwa damu ya Kigeni; Mengineyo: Tarehe na sababu ya kufa, kuchinjwa, kuuzwa

## 2. Kumbukumbu za ukuaji (Uzito wa watoto)

Wafugaji wenye mizani inafaa wapime uzito wa mbuzi wao mara moja kila mwezi ili kufuatilia ukuaji wao. Mfano ufuatao unaonyesha jinsi ya kuandika kumbukumbu za uzito wa mbuzi

| Namba ya mbuzi | Tarehe ya kupima na uzito (Kilo) | | | | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|
| | 05.06.2013 | 05.07.2013 | 05.08.2013 | 05.09.2013 | |
| SUA. 251 | 4.50 | 5.2 | 6.6 | 7.1 | |
| SUA. 168 | 14.2 | 14.9 | 15.6 | - | Ameuzwa |
| SUA. 720 | 3.1 | 4.6 | - | - | alikufa 20.07.2013 |

## 3. Kumbukumbu za chanjo na matibabu

Ili kufahamu gharama za matibabu na chanjo, mbuzi gani wana matatizo gani ya afya, lini na mbuzi gani walipata dawa fulani, magonjwa gani yanaleta hasara zaidi, ni vyema kumbukumbu hizi zitunzwe kama inavyoelekweza hapa chini.

| Tarehe | Namba ya mbuzi | Chanjo/ugonjwa | Dawa | Mganga | Sahihi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

## 4. Kumbukumbu za utoaji/uzalishaji maziwa

Ni muhimu sana kufahamu mbuzi jike alizaa lini, ni mzao wa ngapi, anatoa maziwa kiasi gani kila mwezi mpaka kukaushwa na tarehe ya kuacha kukamuliwa. "Ukirekodi" kiasi cha maziwa anachotoa mbuzi kila siku, utaelewa na kuwa na uhakika zaidi juu ya uwezo

wa mbuzi wako katika kutoa maziwa. Miradi mingine hupendelea kurekodi maziwa katika siku moja tu ya mwezi. Katika mradi wa Mgeta ushauri ulitolewa kuwa maziwa yapimwe katika siku moja tu kwa wiki. Baada ya kumkausha mbuzi inafaa kuweka muhtasari wa kumbukumbu za kipindi chote alichokamuliwa, kwa mfano:

- Namba ya mbuzi
- Tarehe ya kuzaa
- Kiasi cha maziwa kila mwezi
- Jumla ya maziwa katika kipindi kizima cha kukamuliwa
- Tarehe ya kuacha kumkamua
- Idadi ya siku alizokamuliwa.

## 5. Kumbukumbu za upandishaji

Uwekaji wa kumbukumbu za upandishaji ni muhimu ili:

- Kufahamu mbuzi amepandishwa kwa mara ya kwanza kwenye umri gani.
- Mfugaji mwenye tatizo la kujua dalili za joto anaweza kutumia kumbukumbu kufuatilia upataji wa joto wa mbuzi.
- Kufahamu mbuzi ambao wana matatizo ya kupata mimba.

Mfano wa kumbukumbu za upandishaji ni kama ifuatavyo:

| **Namba ya mbuzi** | **Tarehe Joto la 1** | **Dume** | **Tarehe Joto la 2** | **Dume** | **Tarehe Joto la 3** | **Dume** | **Tarehe ya kuzaa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

Mbuzi anayerudia joto zaidi ya mara tatu aandikwe upya.

Kumbukumbu nyinginezo

**Hizi ni kama zifuatazo:**

- Manunuzi na matumizi mbalimbali kama dawa, madini, na pumba.
- Mauzo ya mbuzi (ameuzwa lini, wapi, kwa matumizi gani, na kwa kiasi gani)
- Kuhasi dume, kumwachisha mbuzi mtoto maziwa na mengineyo.

Kinachohitajika ni kuandika tarehe na shughuli iliyofanyika siku hiyo. Kwa mfano:

| Tarehe | Maelezo |
|---|---|
| 20.08.2013 | Niliuza dume namba SUA. 121 kwa Mr. Kifaro kwa Shs. 120,000/= |
| 12.09.2013 | Nilihasi dume namba SUA. 186 |

## Jinsi ya kutumia kumbukumbu

## Mfugaji

- Angalia ukuaji wa mbuzi na utoaji maziwa. Kama vitakuwa duni ina maana ulishaji wa mfugaji sio mzuri.
- Tarehe za kuzaliwa zitasaidia kuelekeza ni lini mbuzi jike apandishwe kwa mara ya kwanza.
- Tarehe za joto zitakuonyesha lini mbuzi atategemewa kurudia joto ikiwa hakupata mimba.
- Mapato na matumizi katika mradi yatakuonyesha faida au hasara ya kutunza mbuzi wa maziwa.
- Habari mbalimbali zitasaidia kufanya uchaguzi wa mbuzi bora katika kundi.

## Bwana mifugo

- Kumbukumbu zikiangaliwa vizuri zimtasaidia afisa ugani (bwana mifugo) kutoa ushauri sahihi kwa mfugaji.
- Pia kumbukumbu zitasaidia kutambua matatizo makubwa ya mbuzi wa maziwa katika maeneo yetu kwa mfano magonjwa, madawa, upungufu wa madini, matatizo ya kuzailiana kiukoo na shida zingine zitakazohitaji ufumbuzi na/au utafiti.

**KUMBUKUMBU NI MWANGA WA KUTUONYESHA TUTOKAKO NA DIRA YA KUTUONYESHA TUENDAKO KATIKA UFUGAJI WA MBUZI WA MAZIWA.**

# SEHEMU YA TATU

## AFYA YA MBUZI WA MAZIWA

## SURA YA KUMI

# Dalili Za Mbuzi Mgonjwa

### Kutofautisha mbuzi mgonjwa na mwenye afya nzuri

(a) Kumtambua mbuzi wa maziwa mwenye afya nzuri:

- Anakula chakula vizuri.
- Nywele zake zimelala vizuri, zinang'aa na zinapendeza.
- Amechangamka, anatembea na kurukaruka bila tatizo.
- Kama anakamuliwa, anatoa maziwa vizuri.
- Vipimo vyake vya mwili vitakuwa kama ifuatavyo:
  - ✧ Joto la mwili: 38.5 – 39$^{0}$C
  - ✧ Mapigo ya moyo: 70 – 80 kwa dakika moja, haraka zaidi kwa watoto
  - ✧ Kupumua: 22 – 26 kwa dakika moja, haraka zaidi kwa watoto.

(b) Mbuzi mgonjwa anaonyesha dalili zinazolingana na aina ya ugonjwa, lakini kwa kawaida.

- Hali chakula vizuri.
- Nywele zinavurugika, zimesimama na hazipendezi.
- Hachangamki (anazubaa) na kudhoofika.
- Kiasi cha maziwa hushuka, kwa mbuzi anayekamuliwa.
- Anajitenga kutoka katika kundi.
- Vipimo vya mwili vinaweza vikabadilika (lakini sio lazima).

## Jinsi ya kuhakikisha mbuzi ana afya nzuri

- Ni lazima mbuzi apewe lishe bora.
- Usafi wa banda, hori la chakula na vyombo vya kunywea maji.
- Mazoezi (mbuzi aruhusiwe kutembea tembea)
- Kumpatia kinga kwa magonjwa muhimu yanayoathiri afya ya mifugo hapa nchini.
- Uchunguzi wa mbuzi kila siku
- Tiba sahihi ya magonjwa yoyote mara tu yanapotokea.

## Maana ya kinga

Kinga ni utaratibu na hatua maalum zinazochukuliwa kwa madhumuni ya kuhakikisha mnyama hapatwi na ugonjwa au madhara ya afya. Inahusu kuhakikisha yafuatayo:

- Mnyama anakuwa na afya nzuri muda wote.
- Mnyama anapata sindano za kinga kwa magonjwa muhimu
- Usafi wa mazingira anakoishi mnyama unazingatiwa.

**MBUZI NI MNYAMA MGUMU SANA KUUGUA, LAKINI AKIUGUA NI VIGUMU KUTIBIKA. HIVYO NI VIZURI WAKATI WOTE KUELEWA KWAMBA KINGA NI BORA KULIKO TIBA**

## Aina za magonjwa ya mbuzi wa maziwa

Magonjwa muhimu ya mbuzi wa maziwa yanaweza kutengwa kwenye makundi yafuatayo (kwa urahisi wa maelezo).

- Matatizo ya minyoo, magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo.
- Magonjwa hatari yanayoambukiza yaletwayo na virusi, bakiteria na vimelea vya damu.
- Magonjwa mengine.
- Matatizo ya dharura na ajali na

- Magonjwa ya watoto wa mbuzi.

Tunasema magonjwa muhimu kwa sababu mara kwa mara yanashambulia mbuzi na kusababisha hasara kubwa kwa mfano:


- Kuchelewesha ukuaji wa mbuzi wadogo (Kudumaa).
- Kukosa maziwa (utoaji maziwa hupungua au maziwa kukosekana kabisa).
- Kupoteza uzito (hivyo kukosa nyama).
- Kuongezeka kwa gharama za matibabu.
- Vifo vya mbuzi wagonjwa.
- Magonjwa mengine yanaambukiza binadamu.

## SURA YA KUMI NA MOJA

# Athari za Minyoo, Kupe na Ndorobo

### Minyoo

Mbuzi hupata minyoo kwa kumeza majani yenye minyoo michanga iliyoanguliwa toka mayai ya minyoo. Minyoo huishi kwenye tumbo la mbuzi mpaka kufikia umri wa kutaga mayai, ambayo hutoka nje kwa njia ya kinyesi na kuendelea kumea kwa minyoo. Kuna aina mbalimbali za minyoo kwa mfano minyoo ya tumbo, ya mapafu, na ile ya maini. Minyoo humshambulia mbuzi mara nyingi kuliko magonjwa mengine na hasa huongezeka wakati wa masika. Kielelezo namba 11, kinaonesha mzunguko wa jumla wa maisha ya minyoo.



**Kielelezo Na. 11. Mchoro kuonyesha mzunguko wa maisha ya minyoo**

Mbuzi mwenye minyoo hutambuliwa kwa kuwa na afya mbaya, nywele zilizosimama na zisizopendeza, ukuaji mbaya (kudumaa) kwa mbuzi mdogo na utoaji mdogo wa maziwa kwa mbuzi wanaokamuliwa. Ulaji wa chakula huweza kuwa wa kawaida ila mbuzi wadogo wanaweza kuharisha na kupungukiwa damu.

Kwa sasa dawa za kutibu minyoo zinapatikana kwa urahisi na zipo za aina nyingi. Mbuzi hutibiwa kufuatana na aina ya minyoo.

Ili kuzuia minyoo ni vizuri mbuzi wapatiwe **dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu**, hasa wakati wa masika. Watoto wa mbuzi wapewe dawa za minyooo kila mwezi. Vilevile yafaa kuacha kuchungia mbuzi sehemu moja kwa muda mrefu. Mbuzi wachungwe kwenye maeneo makubwa na siyo karibu na nyumba za watu.

## Kuhara (Coccidiosis)

Kuna aina ya vimelea vinavyoshambulia utumbo inayosababisha mbuzi kuharisha, hasa mbuzi wadogo ambao wasipopata matibabu, mbuzi huweza kufa. Mbuzi wenye ugonjwa huu huharisha kinyesi chenye damu, hupoteza uzito haraka na hufa kwa wingi kutokana na ukosefu wa maji na chumvi chumvi mwilini.

Ugonjwa huu hutibiwa kwa dawa, maji ya chumvi chumvi yaliyoongezwa sukari kidogo (kama ikipatikana), dawa za "antibiotic" (kwa mfano amprolium) na salfa.

Kuzuia ugonjwa huu ni kwa kuzingatia usafi wa mzingira na vyombo vya maji na chakula. Pia mbuzi wasirundikwe wengi kwenye eneo dogo.

## Magonjwa yanayoenezwa na kupe na ndorobo

### (a) Ndigana baridi (Anaplasmosis)

Ugonjwa huu ni hatari zaidi kwa ng'ombe. Mara nyingi mbuzi hawaoneshi dalili za ugonjwa huu lakini wanaugua mara kwa mara. Ndigana baridi inasababishwa na bakiteria aina ya riketsia na kusababisha mbuzi kukosa nguvu kukonda na kukosa damu (anemia). Ugonjwa unaweza kuonesha dalili za homa, kutokula chakula vizuri, kukonda, njano sehemu zote laini za mwili hasa za ndani, kutupa mimba na vifo. Ugonjwa unaweza kuenezwa na kupe na vifaa vichafu vya kudungia sindano. Hutibiwa kwa antibiotic (mfano Tetracycline).

Ni vyema na muhimu sana kuwakinga wanyama dhidi ya ugonjwa. Unaweza kuwakinga kwa kudunga sindano za chanjo (kinga), lakini pia kwa kuwaogesha mbuzi kwa dawa za kuua kupe mara moja au mbili kwa wiki.

### (b) Mkojo mwekundu (Babesiosis)

Ni ugonjwa hatari unaosababishwa na vimelea vya damu (blood parasites) vinavoitwa Babesia na hushambulia na kuharibu chembechembe nyekundu za damu. Mbuzi wanaugua mara kwa mara. Ugonjwa huu husababisha hasara kubwa hasa kukosa maziwa, kuongeza gharama za matibabu na vifo vya mbuzi.

Dalili za ugonjwa huu zinaweza zisionekane waziwazi, lakini kwa kawaida mbuzi wagonjwa huwa na homa kali, hushindwa kula chakula vizuri kudhoofika, kama wanakamuliwa utoaji maziwa hupungua, macho huwa mekundu, sehemu zote laini hasa za ndani hugeuka kuwa njano, hukojoa mkojo mwekundu, hutupa mimba na hatimaye mbuzi hufa.

Ugonjwa wa mkojo mwekundu unaenezwa na kupe, hivyo ni muhimu sana kuogesha mbuzi kwa dawa za kuua kupe mara moja au mbili kwa wiki. Tiba ya ugonjwa huu ni kwa kutumia dawa za antiobiotics na dawa nyinginezo.

### (c) Ndigana makata ya mbuzi na kondoo

Huu ni pia ugonjwa hatari wa ng'ombe, kondoo wa mbuzi unaosababishwa na vimelea vya damu (*Theileria hirci*) na kuenezwa na kupe. Mbuzi wanapata ugonjwa huu mara chache.


Dalili muhimu za ugonjwa huu ni homa kali, kutokwa na makamasi, majimaji machoni, puani na povu mdomoni kuvimba tezi zote zilizo chini ya ngozi, kuharisha, kukonda na kufa. Ugonjwa huu unatibiwa kwa dawa za Butalex, Terit na Tetracycline. Unaweza kuzuilika kwa kuwaogesha mbuzi kwa dawa za kuua kupe.

### (c) Ugonjwa wa malale (Trypanosomiasis)

Ni ugonjwa hatari sana wa mbuzi, kondoo na wanyama wengine unaosababishwa na vimelea vya damu (Trypanosoma) na kuenezwa na ndorobo (Kielelezo Na. 12).

Ndorobo (mbung'o) ni aina ya inzi ambao wanapendelea kukaa katika misitu minene, kwenye vichaka, kando kando ya mito, mifereji na mabonde ya maji. Mfano mzuri wa maeneo wanakopatikana mbung'o ni kama pori la Mikumi. Dalili za ugonjwa ni homa, mnyama kutokula chakula vizuri, kupunguza utoaji maziwa, kutoa kinyesi kilichochanganyika na damu, damu kutoka puani, kutokwa na nywele mwilini hasa sehemu za mkia na vifo kama matibabu hayakupatikana.

Ugonjwa huu unaweza kutibiwa na dawa aina ya Berenil, Novidium na Samorin. Kati ya mbinu za kuzuia ugonjwa huu ni pamoja na kutumia sindano za kinga za Samorin kila baada ya miezi mitatu na kupunguza vichaka na misitu karibu na nyumba za mbuzi ili kuepukana na mbung'o. Kuwaogesha mbuzi kwa dawa ya kupe aina ya pyrexin (pareto) pia huzuia na kuua ndorobo. Mbung'o na vimelea wameoneshwa katika Kielelezo namba 12.



**Kielelezo Na. 12. Picha ya Ndorobo na vimelea vya damu (Trypanosoma).**

SURA YA KUMI NA MBILI

# Magonjwa Hatari Yanayoambukiza

## Kichaa cha Mbwa (Rabies)

Ni ugonjwa hatari sana wa mbwa lakini pia huwapata wanyama wengine kama mbuzi na kondoo. Unashambulia ubongo na kusabishwa na virusi. Mbuzi anaugua baada ya kuumwa na mnyama mwenye kichaa cha mbwa. Mate ya mnyama ndiyo yenye virusi vya ugonjwa.

## Dalili zake

(a) Kichaa cha kuzubaa – Kukaza (kupooza) misuli ya koo, kushindwa kumeza, kutokwa mate mdomoni, kulegea taya la chini na hata kifo.

(b) Kichaa cha ukali – kubadilika kwa tabia ya mbuzi, kuogopa na kushtuka, kushambulia na kuuma ovyo vitu vya kawaida, kumeza mawe, vijiti, kuvunja maeneo na kupiga kelele sana. Mbuzi anakuwa mkali na wakati wowote yuko tayari kufanya mashambulizi. Hatimaye mbuzi hufa.

Ugonjwa huu hauna tiba, ila kuna kinga. Ni muhimu kuwadunga mbuzi sindano za kinga (chanjo) za kichaa cha mbwa kila mwaka hasa katika maeneo yenye ugonjwa huu mara kwa mara. Pia ni muhimu kudunga mbwa na paka wote sindano za kinga za ugonjwa wa kichaa cha mbwa na kupiga kampeni ya kuua mbwa wanaozurura ovyo.

**TAHADHARI**

(a) Endapo binadamu ataumwa na mbwa mwenye kichaa ni vyema mara moja adunge sindano maalum za kuzuia ugonjwa huu zinazotumika kwa binadamu. Sindano hizo zinapatikana hospitalini au zahanati.

(b) Endapo mbuzi ataumwa na mbwa au paka ni vizuri mbwa au paka aliyemuuma afuatiliwe kwa makini. Kuwa makini sana na mbuzi aliyeumwa.

(c) **HAIRUHUSIWI KABISA KULA NYAMA YA MBUZI MWENYE KICHAA CHA MBWA.**

## Homa ya bonde la ufa [Rift Valley Fever (RVF)]

Ni Ugonjwa wa mbuzi, kondoo, ng'ombe na hata binadamu ambao unasababishwa na virusi na huambukiza kwa haraka. Ugonjwa huu huenezwa na mbu na utokeapo husababisha homa kali, kuharisha na vifo vingi vya ghafla. Mpaka sasa RVF haina tiba na hivyo inasisitizwa sana mbuzi wapate sindano za kinga kila mwaka ili kuzuia ugonjwa huu usitokee. Pia ni vizuri kuchunguza afya ya mbuzi mara kwa mara hasa wakati wa mbu wengi na kuongeza jitahada za kupambana na mbu ama kutumia kinga wakati wa mlipuko unapotokea.

## Ugonjwa wa Nairobi wa Kondoo (Nairobi Sheep Disease)

Ni ugonjwa wa kondoo na mbuzi unaosababishwa na virusi na kuenezwa na kupe. Ugonjwa huu husababisha vifo vingi. Dalili zake ni homa kali, kutokwa makamasi mazito puani, kuharisha kinyesi chenye damu kinachonuka sana, na maumivu wakati wa haja kubwa. Ugonjwa huu bado hauna tiba na hivyo kinga ya kuzuia ni muhimu. Mbuzi wapate sindano za kinga kila mwaka na kupe wadhibitiwe kwa kuwauwa ama kwa kuwaogesha wanyama mara kwa mara na maji ya dawa.

## Ugonjwa wa miguu na midomo [Foot an Mounth Disease (FMD)]

Ni ugonjwa hatari wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe na unaambukiza haraka sana. FMD husababishwa na virusi. Mbuzi wagonjwa hutoa mate mengi mdomoni na majimaji puani. Dalili zingine ni vidonda kwenye ulimi, fizi, mdomoni na mbuzi kuwa na homa. Tiba ya uhakika hakuna, ila vidonda hutibiwa kwa dawa za vidonda, pamoja na antibiotics. Inashauriwa kuwa mbuzi wapate dawa za kinga kila mwaka au kila mara mlipuko unapotokea.

## Kimeta (Anthrax)

Ni ugonjwa hatari wa ng'ombe, mbuzi, wanyama wengine na hata binadamu na unaosababishwa na bakiteria. Anthrax huleta hasara kubwa na dalili zake ni homa kali, kuharisha, kutokwa damu nyeusi ambayo haigandi kabisa, na kutoa mimba. Ugonjwa huu husababisha vifo vingi sana. Tiba ni sindano za antibiotics. Ugonjwa huu unaweza kuzuiwa kwa sindano za kinga kila mwaka, usafi wa mazingira na lishe bora.

## Ndui (Orf)

Ndui ni ugonjwa wa ngozi unaoleta vinundu vidogo vidogo kwenye ngozi ya uso na mdomo ambavyo baadaye hupasuka au kuchubuka na kuacha vidonda. Wakati mwingine vinundu hivi huonekana kwenye matiti na miguuni na humfanya mbuzi kuchechemea. Ndui inaweza kupona bila tiba baada ya majuma 2 – 4. Hata hivyo vidonda vinatibiwa kwa dawa za vidonda kwa kusafisha na dawa na kisha kudunga antibiotics. Sindano za kinga hutumika kuzuia ndui hasa sehemu zile zinazofahamika kuwa na ugonjwa huu. Ni muhimu kuweka karantini ugonjwa unapotokea ili ugonjwa usisambae.

## Kutupa Mimba (Brucellosis)

Ni ugonjwa hatari unaoshambulia mbuzi, kondoo, ng'ombe na hata binadamu. Unaosababisha mifugo kutupa mimba na husabishwa na bakiteria.

Binadamu huweza kuupata ugonjwa huu kwa kutumia maziwa yasiyochemshwa vizuri au anapomhudumia mbuzi wakati wa matibabu. Kumsaidia mbuzi hasa wakati wa uzazi mgumu bila kuvaa mavazi au glovu za kujikinga ni hatari zaidi. Dalili za brucellosis ni homa, kuharisha, kukonda, matiti kuugua, mbegu za uzazi za beberu kuugua au kutokuwa sawa, kutupa mimba na kubaki kondo la nyuma. Mara nyingi mbuzi anapata ugonjwa kwa kula chakula au maji yenye bakiteria wa ugonjwa.

Brucellosis haina tiba ya uhakika. Mbuzi anaweza kuonekana amepona lakini anaweza kubakia na ugonjwa muda mrefu sana na hata maisha yake yote. Kama hatagundulika mapema mbuzi wa aina hii ataendelea kuwasambaza bakiteria wa ugonjwa. Ni vizuri wanyama wenye ugonjwa huu watengwe na kuchinjwa kwa ajili ya nyama wakati hawaonyeshi dalili za homa. Ugonjwa huu unaweza kuzuilika kwa sindano za kinga dhidi ya ugonjwa, kutekeleza taratibu zote za karantini mara ugonjwa unapoonekana, na kuzingatia lishe bora.

### TAHADHARI

Mbali na Brucellosis, utupaji mimba unaweza kusababishwa na sababu nyingine nyingi. Magonjwa ya virusi, minyoo na yale yanayoenezwa na kupe, ajali kama kupigwa, kula sumu, matumizi mabaya ya dawa za kinga na sababu zingine zaweza kusababisha utupaji mimba kwa mbuzi.

**LAKINI mara kondo la nyuma la uzazi linapobakia ni vizuri kufanya uchunguzi wa Brucellosis na hasa kwa vipimo na kisha kuchukua tahadhari zote ili kuepukana nao.**

## TB (Tuberculosis)

TB ni ugonjwa sugu, hatari na mgumu sana kugundulika. TB inaambukiza wanyama na binadamu na husababisha hasara kubwa kwa mfugaji. Binadamu anaweza kupata ugonjwa huu kwa kunywa maziwa yasiyochemshwa vizuri au kwa kula nyama ya mbuzi mgonjwa.

**TAHADHARI**

Inashauriwa kuchukua tahadhari ya kutokunywa maziwa ya mbuzi/ng'ombe bila kuchemsha na kutokula nyama ambayo haikukaguliwa na daktari/bwana mifugo.

SURA YA KUMI NA TATU

# Magonjwa Mengine

## Ugonjwa wa kiwele (Mastitis)

Ugonjwa wa kiwele unashambulia ziwa la mbuzi na kusababisha uvimbe na maumivu ya kiwele. Pia husabisha kupungua au kuacha kabisa utoaji maziwa. Binadamu anaweza kuambukizwa ugonjwa huu. Kama watoto wa mbuzi watatumia maziwa ya mbuzi mgonjwa, huharisha sana. Mastitis inasababishwa na bakiteria wanaoweza kujipenyeza ndani ya ziwa kupitia jeraha. Bakiteria hawa pia wanaweza kusababishwa na wadudu wanaouma, ukamuaji mbaya au wanaotokana na magonjwa mengine hatari mbalimbali kama TB, Brucellosis, FMD, na mengineyo.

Dalili za mastitis ni ziwa kuvimba na kuwa na joto kali wakati wa mwanzo, ziwa hutoa usaha, mbuzi huonyesha kupata maumivu ziwa lake linapoguswa na maziwa kuganda au kukatika haraka wakati wa kuchemsha. Ugonjwa ukiwa sugu ziwa huwa gumu na mbuzi asipotibiwa anaweza kufa.

Tiba ya mastitis ni sindano za antibiotics kwenye misuli au ndani ya ziwa baada ya kukamua maziwa yote au usaha ulioko ndani ya ziwa. Tiba huendelea kwa siku 5 – 7.

| TAHADHARI |
| --- |
| **Baada ya kutumia antibiotics, maziwa yasitumike kwa siku zisizopungua tatu, kuruhusu dawa kutoka mwilini.** |

Namna ya kuzuia mastitis ni kuzingatia ukamuaji safi na mzuri wa maziwa. Baadhi ya mambo ya kuzingatia katika ukamuaji safi ni pamoja na usafi wa mikono ya mkamuaji, usafi wa vyombo na vifaa vyote vinavyohusika katika ukamuaji, malazi safi ya mbuzi muda wote, kuosha chuchu zote kwa dawa na maji safi kabla na baada ya kukamua maziwa, kutibu mbuzi wagonjwa na kutenga na kuuza wagonjwa sugu ili wachinjwe kwa ajili ya nyama.

## Ugonjwa wa macho

Ugonjwa wa macho ya mbuzi unaletwa na sababu mbalimbali ikiwemo virusi, bakiteria, minyoo, ajali, uchafu machoni, na mengineyo. Ugonjwa unaweza kuambukiza kulingana na sababu iliyouleta.

Dalili za ugonjwa ni macho kutoa machozi au usaha, maumivu, joto na macho kuvimba. Ugonjwa unaweza kuenezwa pia na wadudu wanaoruka kama vile inzi, au kugusana na mbuzi mgonjwa kulingana na kilichousababisha ugonjwa. Tiba ya ugonjwa itafaa sana endapo tatizo lililosababisha ugonjwa litachunguzwa na kutatuliwa. Safisha macho kwa dawa na weka dawa ya antibiotics ya kuminyia machoni.

Kinga izingatie chanzo cha ugonjwa. Pia ni vizuri kuzingatia usafi wa mazingira wanaokoishi mbuzi, kuzuia mchanganyiko wa mbuzi wagonjwa na wazima, kuchunguza mbuzi mara kwa mara kwa matatizo ya macho na kutibu magonjwa.

## Ugonjwa wa kifua (Nimonia)

Ni ugonjwa muhimu sana wa mbuzi wa maziwa ambao unasababishwa na upepo wa baridi, mazingira ya unyevunyevu na bakiteria. Mbuzi wanaugua mara kwa mara.

Dalili za nimonia ni pamoja na homa, kuhema kwa taabu na haraka, kukohoa, kutokwa makamasi na povu puani na mdomoni na vifo vya ghafla au vya baada ya muda mrefu bila matibabu. Tiba ni antibiotics za sindano za kwenye misuli. Mbuzi wagonjwa wawekwe kwenye sehemu yenye joto na kavu bila upepo wala baridi.

Ili kuzuia nimonia, hakikisha banda la mbuzi halivuji, wala halipitishi baridi kali au upepo. Mbuzi wagonjwa watengwe.

## Kuoza kwato (Foot rot)

Ni ugonjwa muhimu sana wa mbuzi ambao huonekana wakati wa mvua nyingi au kama mbuzi anakaa sehemu zenye unyevunyevu, uchafu mwingi, matope au zenye maji machafu. Sababu zingine ni kuchomwa na miiba au misumari. Mbuzi wanaugua mara kwa mara.

Dalili za ugonjwa huu ni mbuzi kuchechemea, kwato kuvimba na kutoa usaha. Pia kwato huwa na joto kali. Tiba ya ugonjwa ni kuosha kwato kwa dawa au maji safi na sabuni, kukamua kwato ili kuondoa usaha wote, kupuliza kwato za mbuzi kwa antibiotics na kupiga sindano ya tetanus.

Ili kuepukana na ugonjwa huu ni pamoja na kutowaruhusu mbuzi kusimama kwenye matope na kuzingatia usafi wa uhakika wa mazingira ya mbuzi.

## Kuvimbiwa (Bloat)

Kuvimbiwa ni tatizo la tumbo kuvimba kutokana na mchafuko wa tumbo ambalo hutoa hewa au povu jingi katika mojawapo ya matumbo ya mbuzi na hivyo kumfanya mbuzi kushindwa kutoa hewa/povu kwa njia ya kawaida. Kuvimbiwa husababishwa na kula

majani mengi mateke yenye asili ya kunde, kuziba kwa njia ya kupitishia chakula toka kinywani hadi tumboni, kula pumba na nafaka kwa wingi, kula sumu na sumu ya nyoka.

Dalili za kuvimbiwa ni pamoja na uvimbe wa tumbo upande wa kushoto, kukosa raha, kulala na kuamka mara kwa mara, pumzi ya haraka na ya shida, kutoka mate na vifo vya ghafla. Unaweza kumtibu mbuzi kwa kumnywesha mbuzi mafuta ya kupikia au maji ya chumvi, kutoboa tumbo la chakula na kutoa hewa kwa kutumia sindano maalum (trocar) au kisu chembamba. Inashauriwa kutolisha kwa wingi vyakula vinavyoweza kuvimbisha tumbo kama vile majani mateke na pumba kwa wingi. Hakikisha majani mateke yanachanganywa na majani makavu.

## Ugonjwa wa tumbo la uzazi (Endometritis)

Ugonjwa huu hutokea baada ya mbuzi kuzaa na vijidudu vya magonjwa kupenyeza ndani ya tumbo la uzazi. Husababishwa na uzazi mgumu, kumsaidia mbuzi katika mazingira machafu, mbuzi kubakisha ndani kondo la nyuma au kondo hilo kuning'inia nje ya uke kwa muda mrefu na sababu nyingine.

Dalili za ugonjwa ni pamoja na kutoa uchafu wenye harufu mbaya kwenye uke, mbuzi kutoingia kwenye joto kama kawaida na kudhoofika. Tiba ni kutoa kondo la nyuma, kuosha uzazi kwa dawa na kutumia vidonge vya antibiotics. Namna ya kuzuia ugonjwa ni pamoja na kumzalisha mbuzi katika mazingira ya usafi na kuwa mwangalifu na kuwa karibu na mbuzi wakati wa kuzaa.

## Majipu na vidonda

Majipu na vidonda vyaweza kumpata mbuzi wakati wowote wa uhai wao na vinawapata makundi mbalimbali ya mbuzi. Majipu na vidonda vinaweza kusababishwa na wadudu ama ajali. Ni muhimu



kuhakikisha kwamba uchafu wo
kwenye jipu umesafishwa kwa
(disinfectants) kama Hydrogen
kutumia maji safi na sabuni. Ba
antibiotics (spray) na kama ita
vifungwe bendeji.

## Wadudu wa ngozi (kupe, viro

Kupe, viroboto, chawa, na ut
wanaonyonya damu na hivyo kue
na pia husababisha maumivu na
wanaweza kudhibitiwa kwa kuog
moja au mbili kwa wiki na kunyun
mahali wanakolala mbuzi.

kuhakikisha kwamba uchafu wote kwenye vidonda na usaha kwenye jipu umesafishwa kwa dawa za kusafishia vidonda (disinfectants) kama Hydrogen Peroxide na lodine, au kwa kutumia maji safi na sabuni. Baada ya vidonda kukauka tumia antibiotics (spray) na kama itaonekana vyema basi vidonda vifungwe bendeji.

## Wadudu wa ngozi (kupe, viroboto, chawa, utitiri)

Kupe, viroboto, chawa, na utitiri ni wadudu wabaya sana wanaonyonya damu na hivyo kueneza magonjwa mengi ya hatari na pia husababisha maumivu na kuharibu ngozi. Wadudu hawa wanaweza kudhibitiwa kwa kuogesha na dawa za wadudu mara moja au mbili kwa wiki na kunyunyuza dawa ya unga (servin dust) mahali wanakolala mbuzi.

# SURA YA KUMI NA NNE

# Jinsi ya kukabiliana na Matatizo ya Dharula (Ajali)

## Sumu katika chakula

Sumu inaweza kuwa mimea kama mihogo michungu, machipukizi ya mtama, maua, matunda ya miti, ndulele na miti mingine, pia katika vyakula vya nafaka vilivyoharibika kutokana na utunzaji mbaya au madawa ya sumu.

Dalili za mnyama kuwa na sumu hutegemea na wingi wa sumu iliyoliwa. Sumu huweza kusababisha vifo vya ghafla, maumivu ya tumbo, kuhara, kutoa povu kinywani, kutetemeka, kizunguzungu na mapigo ya moyo kuongezeka. Tiba ya haraka ni kumnywesha mbuzi maziwa halisi na maji ya chumvi. Kama mbuzi amevimba hewa itolewe tumboni. Ili kuzuia mbuzi asile sumu, mfugaji anashauriwa kuhakikisha kwamba mbuzi hawafikii sumu au vyakula vinavyoweza kuwa sumu na hawakai na njaa.

## Kuumwa na nyoka (Snake bite)

Sumu ya nyoka huathiri sana mishipa ya fahamu, damu na mapafu. Ni muhimu sana ikiwezekana nyoka atambuliwe, muda tangu kuumwa mpaka matibabu uwe mfupi iwezekanavyo na sehemu mbuzi alipoumwa itambuliwe.

Dalili za kuumwa na nyoka (sumu ya nyoka) ni pamoja na mbuzi kufa ghafla, mbuzi kuchoka na kubaki nyuma ya kundi, kutoka

damu alipoumwa, kupuma kwa shida, mapigo ya moyo kuongezeka na kutocheua.

Inawezekana kumsaidia mbuzi kwa kujaribu kuondoa meno ya nyoka na kufunga kamba juu kidogo ya jeraha. Jeraha lisafishwe kwa maji safi, na baadaye kwa dawa, kutumia jiwe la sumu kama lipo. Jiwe la kunyonya sumu libandikwe kwenye jeraha na kama litang'ang'ania liachwe mpaka lidondoke lenyewe. Mbuzi anyweshwe maziwa, adungwe sindano za sumu ya nyoka, dawa za tetanus na antibiotics.

Kuumwa nyoka kunaweza kuzuilika endapo mbuzi watachungwa sehemu ambazo hazina nyoka au kutumia njia ya kulishia ndani ya nyumba zao (zero grazing).

TAHADHARI

Mbuzi akiumwa na nyoka kichwani, shingoni, kifuani au tumboni ni rahisi sana kufa. **HAIRUHUSIWI KULA NYAMA YA MBUZI ALIYEUMWA NA NYOKA.**

## Kuvunjika miguu au mifupa

Ni tatizo linatokea baada ya mbuzi kupigwa na mtu kwa fimbo au jiwe, mbuzi kupigwa na mbuzi mwingine au mbuzi kuanguka. Kuvunjika miguu kunaweza kuambatana na ngozi au misuli kuchanika. Kama mbuzi atakuwa anatokwa damu baada ya ajali au kuvunjika, mfugaji ajitahidi kusimamisha damu hiyo kwa kuufunga mguu juu kidogo ya sehemu iliyovunjika. Pia barafu au kitambaa kilichotumbukizwa kwenye maji baridi kitumike kufunga kidonda baada ya kuondoa uchafu wote kwa dawa za kusafisha vidonda.

Mifupa iliyovunjika irekebishwe sehemu yake na ifungwe vizuri kwa bendeji na vipande vya mbao au miti ili kuzuia mbuzi asiutumie mguu uliovunjika. Kidonda kisafishwe vizuri, mbuzi apatiwe dawa za kupunguza maumivu, antibiotic na zile za tetanus.

Kuvunjika miguu au mifupa kunaweza kupungua kama mfugaji atasisitiza wasaidizi au wahudumu wa mbuzi wasitumie fimbo au mawe wanapowasimamia mbuzi majumbani au machungani, kuhakikisha mbuzi wanapita kwenye njia nzuri, kuzuia msongamano wa mbuzi wengi kwenye sehemu moja na kuzuia mbuzi wasipigane.

## Kuumwa na nyuki

Tatizo hili hutokea endapo mbuzi wanafungwa kamba au wanachungwa sehemu yenye nyuki. Mbuzi akiumwa na nyuki wengi hupumua kwa shida, mapigo ya moyo huongezeka, mwili huvimba, huwa na harufu ya asali, miiba ya nyuki kuonekana mwili mzima na mbuzi anaweza kufa.

Ili kutibu tatizo la kuumwa na nyuki, dawa za kupunguza maumivu, zile za kuondoa sumu mwilini, dawa za kupaka ili kuondoa uvimbe na miwasho zaweza kutumika.

Inawezekana pia kuzuia mbuzi wasiumwe na nyuki kwa kutowapeleka malisho yaliyo karibu au katika sehemu zenye nyuki.

## Kuungua moto

Mbuzi akipata ajali ya kuungua moto tumia mafuta, antibiotics na dawa za maumivu kulingana na ushauri wa daktari.





# Magonjwa ya Wa

## Kuharisha

Ni ugonjwa wa watoto wa mbuzi u
bakiteria na hasa baada ya kunywa

Dalili ni pamoja na kuharisha kiny
asipopata matibabu hufa baada
kufanya uchunguzi wa maabara na
na kumpa mbuzi maji mengi yenye
Kuharisha kunaweza kuzuilika kwa
mbuzi wadogo na mazingira yanayo

## Mbuzi Mzazi kutojali mtoto kuzaa

Tatizo la mbuzi kumkataa mtoto
kawaida na linaweza kutokea kwa
hili linaweza kusababisha watoto
inayohitajika (starvation) kwa wato
wa joto na ulinzi wa mama wa mbuz

Mfugaji hakikisha unawaweka mb
joto, kuwafunika blanketi au gunia
(glucose) kwa njia ya sindano na
mwanzo ya mbuzi kwa kukamua to

# Magonjwa ya Watoto wa Mbuzi

## Kuharisha

Ni ugonjwa wa watoto wa mbuzi unaosababishwa na minyoo na bakiteria na hasa baada ya kunywa maziwa mengi na machafu.

Dalili ni pamoja na kuharisha kinyesi cha rangi ya njano. Mbuzi asipopata matibabu hufa baada ya siku chache. Ni muhimu kufanya uchunguzi wa maabara na kutumia tiba sahihi. Antibiotics na kumpa mbuzi maji mengi yenye chumvi ni tiba inayoshauriwa. Kuharisha kunaweza kuzuilika kwa kufanya usafi wa vyumba vya mbuzi wadogo na mazingira yanayowazunguka.

## Mbuzi Mzazi kutojali mtoto/watoto wake baada ya kuzaa

Tatizo la mbuzi kumkataa mtoto au kutowajali watoto ni la kawaida na linaweza kutokea kwa mbuzi wakati wowote. Tatizo hili linaweza kusababisha watoto kupata njaa na kukosa lishe inayohitajika (starvation) kwa watoto na pia kusababisha ukosefu wa joto na ulinzi wa mama wa mbuzi kwa watoto wake.

Mfugaji hakikisha unawaweka mbuzi watoto kwenye sehemu ya joto, kuwafunika blanketi au gunia safi, kuwapatia maji ya sukari (glucose) kwa njia ya sindano na kuendelea kuwapa maziwa ya mwanzo ya mbuzi kwa kukamua toka kwa mama.

## Njia ya kinyesi kufunga

Hili ni tatizo la kuzaliwa ambalo hutambulika wakati mbuzi aliyezaliwa anachunguzwa kama ana kasoro. La kufanya ni kupasua ngozi ya juu iliyofunika njia hiyo kwa kutumia wembe msafi (mpya).

## Jipu la kitovu

Kitovu huvimba na kutoa kwanza maji maji na kisha usaha. Homa kali na vifo vyaweza kutokea baada ya siku chache. Ugonjwa huu husababishwa na aina mbali mbali za bakiteria.

Unaweza kuwatibu mbuzi kwa kusafisha kitovu kwa dawa za kuosha vidonda na kuweka antibiotic kwenye kitovu, na pia kutumia sindano. Safisha kitovu na kupaka dawa ya vidonda na kufanya usafi wa vyumba vya mbuzi wakati wote.





# Matumizi y

Ni muhimu mfugaji wa mbuzi aelewe
ya dawa zinazotumika kutibu magon
mbuzi, kwa sababu mara nyingine
dawa hizi mwenyewe pale ambapo a
mifugo au bwana mifugo.

## Upatikanaji na matumizi ya da

Dawa za kinga (chanjo) kwa mago
hatari haziuzwi madukani. Hizi hut
uliowekwa na serikali na hupatikana
na mkoa. Matumizi yake ni baada
mifugo au bwana mifugo.

Dawa aina ya antibiotics zinatumika
virusi, vimelea, na mengineyo. A
maduka ya dawa lakini inashauriwa
kuelekezwa na daktari wa mifugo i
inafaa kutumika kwa ugonjwa aina
kumpatia mbuzi mgonjwa na muda.
mbuzi apewe dawa mara ngapi kwa
vema kufanya hivyo kwa sababu
antibiotics, na kila moja ina nguvu
bakiteria, vimelea, virusi na wa
magonjwa mbalimbali. Vilevile
kusababisha vijidudu kuzoea dawa
na manufaa.

SURA YA KUMI NA SITA

# Matumizi ya Dawa

Ni muhimu mfugaji wa mbuzi aelewe machache kuhusu matumizi ya dawa zinazotumika kutibu magonjwa au maradhi mengine ya mbuzi, kwa sababu mara nyingine mfugaji atalazimika kutumika dawa hizi mwenyewe pale ambapo atakosa huduma ya daktari wa mifugo au bwana mifugo.

## Upatikanaji na matumizi ya dawa

Dawa za kinga (chanjo) kwa magonjwa muhimu au magonjwa hatari haziuzwi madukani. Hizi hutolewa kwa utaratibu maalum uliowekwa na serikali na hupatikana katika ofisi za mifugo wilaya na mkoa. Matumizi yake ni baada tu ya ushauri wa daktari wa mifugo au bwana mifugo.

Dawa aina ya antibiotics zinatumika kutibu magonjwa ya bakiteria, virusi, vimelea, na mengineyo. Antibiotics zinapatikana katika maduka ya dawa lakini inashauriwa kuanza kutumika baada ya kuelekezwa na daktari wa mifugo ili kuelewa vizuri ni dawa gani inafaa kutumika kwa ugonjwa aina fulani na kiasi cha dawa cha kumpatia mbuzi mgonjwa na muda. Kwa mfano ni vema kufahamu, mbuzi apewe dawa mara ngapi kwa siku na ni kwa siku ngapi. Ni vema kufanya hivyo kwa sababu kuna aina mbalimbali za antibiotics, na kila moja ina nguvu tofauti katika kupambana na bakiteria, vimelea, virusi na wadudu wengine wanaosabisha magonjwa mbalimbali. Vilevile utumiaji mbaya unaweza kusababisha vijidudu kuzoea dawa hizo na hivyo kuzifanya zisiwe na manufaa.

Kwa upande wa dawa za minyoo, zile za magonjwa yaletwayo na kupe, ndorobo, viroboto, na magonjwa ya aina hiyo zinapatikana kwa urahisi katika maduka ya dawa. Kama zilivyo antibiotics dawa hizi pia zipo za aina nyingi na hivyo ni vizuri kupata ushauri wa daktari wa mifugo kuhusu dawa za kununua na zinazofaa zaidi kwa aina ya minyoo inayohusika. Halikadhalika, dawa za kupe na viroboto zipo nyingi madukani hivyo ni lazima daktari wa mifugo ashauri ni dawa ipi inafaa zaidi. Hii ni kwa sababu kupe wanaweza kuwa sugu kwa aina moja ya dawa, na ikitumiwa itakuwa haileti manufaa yoyote, bali hasara tupu (kupoteza pesa).

Dawa za vidonda au kusafisha vidonda zipo nyingi na kawaida inawezekana kutumia dawa yoyote ile kwa uchaguzi na pendekezo la mfugaji. Hata hivyo siyo vibaya kupata ushauri wa daktari wa mifugo.

> **TAHADHARI**
>
> Kila mara pata ushauri wa daktari wa mifugo kabla ya kutumia dawa ya aina yoyote hasa ukiwa na mashaka.

## Malengo mengine

(a) Sindano na bomba za kudunga dawa kila mara ziwe safi kwa kuchemshwa.

(b) Mbuzi mgonjwa anahitaji mazingira yenye joto la wastani na malazi mazuri yaliyo safi, yaliyotandikwa nyasi kavu.

(c) Inaweza kuwa kazi ngumu sana kumlazimisha mbuzi mgonjwa kula chakula. Endapo ndivyo basi pawepo na maji safi ya kunywa. Kama hataki kunywa maji ni vizuri apewe



glucose (au sukari kijiko kimoja ... (glasi moja) ya maji safi. Mbuzi ... kila baada ya saa nne.

(d) Ikishagundulika mbuzi ni mgonjwa ... wa mifugo au bwana mifugo. ... zaidi wa dawa na matibabu ... lililogundulika. Vilevile watapeleka ... kama ni ugonjwa hatari ambao ... Karantini ni hatua inayochukuliwa ... au mkoa kufuatana na utaratibu ... Karantini ina madhumuni ya kuzuia ... hatari. Ifuatayo ni mifano ya karantini ...

(i) Kuzuia utoaji na uingizaji wa ... lenye ugonjwa. Pia kuzuia ... nje ya eneo husika.

(ii) Kuzuia watu kutoka holela nje ...

(iii) Kuanza chanjo, matibabu na ...

(iv) Kutenga mbuzi wagonjwa na ... zote zinazodhibiti mchanganyiko ... na wa wazima.

(v) Kufanya usafi na kuweka ... wanakoishi mbuzi, kuchoma ... na mizoga yote.

glucose (au sukari kijiko kimoja cha chakula) kwa robo lita (glasi moja) ya maji safi. Mbuzi apewe mchanganyiko huo kila baada ya saa nne.

(d) Ikishagundulika mbuzi ni mgonjwa ni vyema kumwita daktari wa mifugo au bwana mifugo. Wataalam hawa wana ufahamu zaidi wa dawa na matibabu yanayofaa kwa tatizo lililogundulika. Vilevile watapeleka taarifa wilayani au mkoani kama ni ugonjwa hatari ambao unastahili kuwekwa karantini. Karantini ni hatua inayochukuliwa na ofisi ya mifugo wilaya au mkoa kufuatana na utaratibu uliowekwa na Serikali. Karantini ina madhumuni ya kuzuia kuenea kwa magonjwa hatari. Ifuatayo ni mifano ya karantini:

(i) Kuzuia utoaji na uingizaji wa wanyama katika eneo lenye ugonjwa. Pia kuzuia uuzaji mbuzi na mazao yake nje ya eneo husika.

(ii) Kuzuia watu kutoka holela nje ya eneo la ugonjwa.

(iii) Kuanza chanjo, matibabu na uchunguzi wa kina.

(iv) Kutenga mbuzi wagonjwa na kuchukua hatua nyingine zote zinazodhibiti mchanganyiko wa mbuzi wagonjwa na wa wazima.

(v) Kufanya usafi na kuweka dawa kwenye mazingira wanakoishi mbuzi, kuchoma majani, mbolea, takataka na mizoga yote.